SportPesa
TZS. 783,781,040
NI YA KWAKO WIKI HII,
BETI LEO UWE MILIONEA
SPORTPESA.CO.TZ PIGA *150*87#



**Shahidi:** Nilimuuzia Sabaya 'shangingi' kwa mil. 60/-

UKURASA 3




**Dele kuondoka Spurs Januari**

UKURASA 22


# Nipashe

Jumatano Desemba 15, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580795

www.ippmedia.com

twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US




# Warioba aibua kasoro uchaguzi

- **Ataka** zijadiliwe kupata ufumbuzi, asema TCRA, msajili magazeti wamepewa nguvu kubwa... *Endelea ukurasa 2*

## YALIYOMO

UKURASA WA 4
**MAPINGAMIZI UTETEZI KESI MBOWE YAKWAMA**
MAHAKAMA Kuu Divisheni ya Makosa ya Rushwa na Uhujumu Uchumi, imetupilia...

UKURASA WA 7
**KADA CCM AWAKOSOA BULEMBO NA POLEPOLE**
MAKADA wa CCM, Humphrey Polepole na Abdalah Bulembo wametakiwa...

UKURASA WA 7
**USAFIRISHAJI GUNDI NJE WARUHUSIWA**
WAZIRI wa Maliasili na Utalii, Dk. Damas Ndumbaro, ameruhusu kusafirishwa...



Wananchi wakipita kwa shida wakati wa kuingia na kutoka kwenye Soko la Mabibo maarufu "Mahakama ya Ndizi", mkoani Dar es Salaam jana, kutokana na matope yaliyolizingira soko hilo na kusababisha usumbufu mkubwa kwa wateja na wafanyabiashara. **PICHA: MIRAJI MSALA**

## Chanjo mbili mpya corona kuwasili nchini

UKURASA 4



## Hoja 4 ACT- Wazalendo mkutano na Rais Samia

UKURASA 2

**MICHEZO** **YANGA SC NA HASIRA KWA IHEFU** UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6




Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, Abdulmajid Nsekela (kushoto) na Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Ndege la Tanzania (ATCL), Mhandisi Ladislaus Matindi, wakionyesha ishara ya uzinduzi wa huduma ya malipo ya tiketi za ndege za ATCL kupitia mtandao wa Benki hiyo unaojumuisha matawi, CRDB Wakala na SimBanking, jijini Arusha jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Warioba aibua kasoro uchaguzi

**Na Mwandishi wetu**

WAZIRI Mkuu mstaafu, Jaji Joseph Warioba, amesema kasoro zilizojitokeza kwenye Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020 lazima zijadiliwe kwa uwazi ili kuepusha kujitokeza kwenye Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2025.

Pia ameeleza kushangazwa na watu wanaoogopa kujadili kasoro hizo waziwazi, akionya kuwa kitendo hicho kinafanya uchaguzi kuwa wa viongozi na vyama na siyo wananchi ambao ndiyo wanapiga kura.

Jaji Warioba aliyasema hayo jana mkoani Dar es Salaam wakati wa uzinduzi wa Ripoti ya Vyombo vya Habari na Uchaguzi 2020, Ubora wa Maudhui ya Vyombo hivyo Tanzania, uliofanywa na Shule Kuu ya Uandishi wa Habari na Mawasiliano kwa Umma (SJMC) ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM).

Alisema imefika mahali watu wanaogopa kuzungumzia hitilafu zilizojitokeza kwenye uchaguzi wa mwaka 2020, huku akivinyooshea kidole vyombo vya habari kwa kutokufanya uchambuzi kuonyesha kasoro hizo.

Alitoa mfano kuwa aliwahi kufanya kazi idara ya sheria serikalini na ilikuwa ni kawaida kila baada ya uchaguzi kubaini kasoro na kufanya tathmini ili zisijirudie na ndiyo maana sheria na kanuni za uchaguzi zimekuwa zikifanyiwa marekebisho.

"Tumefika mahali tunaogopa kuzungumzia hitilafu tulizoziona kwenye uchaguzi wa mwaka 2020, ni kawaida uchaguzi wowote utakuwa na hitilafu kokote duniani, imefika mahali tunaogopa kuzungumzia hitilafu tulizoziona kwenye mchakato wa uchaguzi.

"Uchaguzi uliopita ulikuwa na hitilafu nyingi sana na zilionekana wazi. Kwa mara ya kwanza nchi hii ilikuwa kama ndiyo tunaanza uchaguzi, hatukuzoea."

"Kwa mara ya kwanza watu (wagombea) wengi wameenguliwa tangu mwaka 1961 nchi ipate uhuru, kasoro zilijitokea nyingi sana lazima tutafute sababu ili yasijirudie.

"Kwa sasa tuzungumze haya (kasoro) yasitokee tena lakini watu wanazungumza chini chini wanaogopa kuyasema, hapana! Lazima tuzungumze tujue uchaguzi ni wa wananchi na taratibu tutakazokuwa nazo ziwe za wananchi na siyo viongozi," alisema.

**VYOMBO VYA HABARI**

Jaji Warioba alisema vyombo vya habari vinatoa habari nyingi lakini bado inahitajika kazi kubwa kwa waandishi kutoa taarifa za kusaidia wananchi badala ya kuwa wanaripoti matukio ya watu.

"Katika ripoti hii tumeona wakati wa kampeni za Uchaguzi Mkuu mwaka 2020 watu walisikiliza na kuangalia na kusoma habari za kampeni kila siku, ni kipindi ambacho wananchi wengi wakati wa taarifa ya habari wanataka wasikilize, lakini ukiona taarifa zinazopewa kipaumbele.

"Vyombo vya habari havikutoa taarifa muhimu za kusaidia wananchi, huwa najitahidi kujua msimamo wa viongozi na vyama mbalimbali wakati wa uchaguzi.

"Tuliingia uchaguzi wa 2020 ilani za vyama vya siasa hazikuwa zinapatikana kwa urahisi, wananchi walitegemea kutoka kwa wagombea lakini kufahamu sera za vyama ilikuwa ngumu maana hazipatikana ila vyombo vya habari vilikuwa na ilani vilipaswa kufanya uchambuzi ili wananchi waelewe," alisema.

Kwa mujibu wa Jaji Warioba, vyombo vya habari vinajielekeza zaidi kuwaandika viongozi na kuwaacha wananchi, jambo ambalo limejitokeza kwenye ripoti hiyo.

"Tunaona viongozi na serikali ndiyo habari tunasahau wananchi, nilitegemea kwenye uchaguzi wa mwaka 2020 maoni ya wananchi yangeonekana kuanzia hatua za uteuzi lakini hayakuonekana licha ya kwamba uchaguzi ni wa kwao," alisema.

Jaji Warioba alisema sababu zinazoelezwa ni weledi ambalo ni jukumu maalumu la kuwafunza waandishi wawe na ujuzi zaidi, na sababu nyingine ni uchumi ambayo ni lazima wawe na ubunifu kujitengenezea mapato kwa kupunguza kutegemea matangazo kutoka serikalini.

Alisema aliwahi kufanya kazi kama mwandishi wa habari kwenye gazeti la Standard ambalo kwa sasa ni Daily News na hawakuwa na mafunzo ya uandishi wa habari, lakini walifundishwa namna ya kuandaa habari na kufanya utafiti.

"Nimesoma Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), kilikuwa kinasifika kwa kutoa mawazo makubwa, sasa wanahabari wanasema kuna woga unatokana na nini?".

"Mhariri mmoja aliwahi kunieleza kwa kina kwamba 'Mzee tukiandika mambo ya kuudhi mahali fulani tunafungiwa, unakuta mlalamikaji ni huyo, mwandaaji mashkata ni huyo, anayehukumu ni huyo huyo.

"Niliwahi kuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Maadili ya Baraza la Habari Tanzania (MCT), tulisikiliza malalamiko ya wananchi kuhusu vyombo vya habari na tulikuwa tunafanya wazi kila mtu anaridhika, malalamiko yalikuwa yanaletwa waziwazi," alisema.

"Kuna taasisi nyingi (Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) na Msajili wa Magazeti zimepewa madaraka, zinayatumia bila uwazi na wakati mwingine zinatoa adhabu kubwa kabisa kuliko ambazo zinatolewa na mahakama.

"Nchi haiwezi kuendelea kama watu wake hawana uhuru... Tunaweza kuwa na maendeleo ya vitu lakini kama watu hawana uhuru wa kutoa mawazo yao hayo siyo maendeleo,"alisema.

Akiwasilisha utafiti huo, Mtafiti kutoka SJMC, Dk. Abdallah Katunzi, alisema vyombo vya habari binafsi viliripoti habari za uchaguzi mkuu kwa wagombea urais kwa asilimia 64 mgombea urais wa CCM na asilimia 42 mgombea wa CHADEMA.

Alisema kwa Zanzibar vyombo vya Tanzania Bara viliripoti kwa ulinganifu kuliko vilivyopo visiwani humo.

Alisema kwa ujumla vyombo vya habari havikuripoti sera za vyama badala yake viliripoti yaliyokuwa yakisemwa na wagombea huku CCM ikiripotiwa zaidi kuliko upinzani.

"Mazingira kabla na baada ya uchaguzi hayakuwa rafiki kwa vyombo vya habari, Gazeti la Tanzania Daima lilifutiwa usajili kabla ya kuanza uchaguzi huku Clouds Radio na TV wakifungiwa kwa siku saba lakini serikali ilitoa sababu," alisema Dk. Katunzi.

# Hoja nne za ACT mkutano na Samia

**Na Christina Mwakangale**

CHAMA cha ACT-Wazalendo kimesema kinakwenda na ajenda nne kwenye kikao cha siku tatu cha wadau wa siasa kupitia Baraza la Vyama vya Siasa kinachoanza leo jijini Dodoma.

Rais Samia Suluhu Hassan anatarajiwa kuwa mgeni rasmi katika mkutano huo, kwa mujibu wa Idara ya Habari (MAELEZO).

Chama hicho kimesema ajenda hizo ni: Mabadiliko ya kikatiba na kisheria; kuhakikisha kuandikwa upya kwa Sheria ya Vyama vya Siasa; maboresho ya Jeshi la Polisi na vyombo vya ulinzi; na kuachiwa huru kwa Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Freeman Mbowe.

Naibu Katibu wa Habari, Uenezi na Uhusiano na Umma wa chama hicho, Janeth Rithe, kwenye taarifa yake jana, alibainisha kuwa wawakilishi wao katika kikao hicho ni Kiongozi wa Chama, Zitto Kabwe, Kaimu Mwenyekiti wa Chama Taifa, Dorothy Semu, Katibu Mkuu, Ado Shaibu na Mwanasheria Mkuu wa chama, Omary Said Shaaban pamoja na Waziri wa Viwanda na Biashara wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Alisema ushiriki wao katika kikao hicho ni baada ya kupokea barua Oktoba 4, mwaka huu, kutoka kwa Msajili wa Vyama vya Siasa, akijibu kwa maandishi hoja zao ambazo alidai zitazingatiwa.

"Ikumbukwe kuwa Msajili wa Vyama vya Siasa alipotangaza kikao cha Wadau wa Tasnia ya Siasa na Mkuu wa Jeshi la Polisi (IGP) Septemba 24 mwaka huu, chama chetu kiliweka bayana kutoshiriki kikao hicho kwa hoja tatu.

"IGP si msimamizi wa kisera wa tasnia ya kisiasa nchini; kutokuwapo kikaoni kwa mawaziri wenye dhamana ya siasa nchini; kugongana kwa ratiba baina ya kikao hicho na Mkutano wa Kitaifa wa Haki, Amani na Maridhiano ulioitishwa na Kituo cha Demokrasia Tanzania," alisema Janeth na kubainisha:

"Baada ya kupokea barua yetu juu ya hoja hizo, tarehe 4 Oktoba, 2021, Msajili alitujibu kwa maandishi na kutuhakikishia kuwa hoja yetu itazingatiwa na wadau wenye dhamana ya usimamizi wa kisera wa tasnia ya siasa wakiongozwa na Waziri Mkuu na mawaziri mbalimbali wenye dhamana watashiriki."

Janeth alisema dhumuni la chama hicho kushiriki kikao ni fursa kisiasa, ikizingatiwa miaka sita iliyopita demokrasia ilikuwa chini, hivyo kikao hicho ni kama jukwaa la kusukuma mabadiliko ya uendeshaji wa siasa nchini.

Katibu Mkuu wa CHADEMA, John Mnyika, akizungumza na waandishi wa habari mkoani Dar es Salaam Jumapili, alisema wamepokea barua ya mwaliko wa mkutano huo, lakini msimamo wao ni kutoshiriki kutokana na kupuuzwa kwa masuala matatu waliyotaka kufanyika kabla.

"Katika kikao cha Kamati Kuu ya chama kilichofanyika kidigitali Oktoba 10 mwaka huu, tulijadili hali ya kisiasa pamoja na maazimio mengine tulijadili kuwa vyama viende kushiriki mazungumzo vikiwa huru kufanya shughuli za kisiasa, vyenye kutimiza haki za kisheria na kikatiba," alisema Mnyika.

Alisema ili kutimiza hayo walitaka mambo matatu kufanyika ambayo ni serikali kutoa tangazo la kusitisha zuio aliloliita haramu la mikutano ya hadhara na shughuli zingine za kisiasa kwa mujibu wa sheria na kanuni.

Pia serikali ifute kesi zote za kisiasa zilizofunguliwa kabla, wakati na baada ya uchaguzi mkuu, na tatu mashtaka dhidi ya Mbowe yafutwe.

"Mpaka ninavyozungumza na nyinyi (waandishi) leo (Jumapili) toka tutoe msimamo wa kikao cha uamuzi wa Kamati Kuu, hakuna tamko lolote lililotolewa ama na Msajili au Baraza la Vyama vya Siasa au kiongozi mwingine yeyote mwandamizi wa serikali kutangaza kuwa zuio la mikutano ya hadhara na shughuli halali za vyama vya siasa limeondolewa," alisema Mnyika.

"Uamuzi wa chama Oktoba mwaka huu wa kutoshiriki mkutano wa wadau wa vyama ulioitwa na Ofisi ya Msajili na Baraza la Vyama vya Siasa upo palepale," alisisitiza Mnyika.

HABARI KITAIFA



Mwanafunzi bora kwenye masomo kidato cha nne katika Shule ya Wasichana Feza, Nancy Elirehema Mejooli, akiweka kumbukumbu ya jina lake kwenye kitaru maalum cha shule hiyo, wakati wa mahafali jijini Dar es Salaam. Kulia ni Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Omary Juma Kipanga. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Shahidi adai kumuuzia Sabaya gari kwa mil. 60/-

**Na Allan Isack**, ARUSHA

MFANYABIASHARA wa magari, Sharif Shahibu (36), amedai kwamba aliuza kwa aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Hai, Lengai Ole Sabaya, gari aina ya Toyota Landcruiser namba T 222 DBW kwa thamani ya Sh. milioni 60.

Mfanyabiashara huyo, mkazi wa Ilala jijini Dar es Salaam, ambaye ni shahidi wa 12 wa Jamhuri katika kesi ya uhujumu uchumi inayomkabili Sabaya na wenzake sita, alitoa madai hayo mbele ya Hakimu Mkazi wa Mahakama ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Arusha, Patricia Kisinda.

Mbali na Sabaya, washtakiwa wengine katika shauri hilo ni Sylvester Nyengu (26), Enock Togolani (41), Watson Mwahomange (27), John Odemba, Jackson Macha (29) na Nathan Msuya (31).

Akiongozwa na Wakili wa Serikali Mkuu, Tumaini Kweka, Shahibu alidai kwamba yeye ni mfanyabiashara wa magari na kwamba alianza kazi hiyo na hadi sasa ameifanya kwa zaidi ya miaka saba.

Shahibu alidai kuwa June Mosi, mwaka huu, majira ya saa 6:00 mchana alipigiwa simu kufika ofisi za Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Makao Makuu kwa ajili ya kutoa maelezo ya biashara ya gari ya Landcruiser waliyofanya na Sabaya.

"Biashara ya gari tulifanya Februari 2, mwaka huu, katika eneo letu la kuuzia magari," alidai shahidi huku akibainisha kuwa katika duka lao la kuuzia magari mtumba na gari aliloliuza kwa Sabaya ilikuwa mali yake likiwa na thamani ya Sh. milioni 90.

Kabla ya kuuza gari hilo kwa Sabaya, aliimuuzia mtu anayeitwa Filikunjombe kwa Sh. milioni 90 na alitoa Sh. milioni 70 na kiasi kilichobaki (Sh. milioni 20) alishindwa kulipa.

"Baada ya Filikunjombe kushindwa kulipa kiasi cha fedha kilichobakia alianza kutangaza kwenye mitandao ya kijamii na kupitia kwa madalali ndipo Sabaya akaona naliuza," alidai shahidi.

Alidai kuwa Februari 2, mwaka huu, alikutana na Sabaya katika 'apartment' ya Black Hood iliyoko Kijitonyama, Dar es Salaam kwa ajili ya kwenda na nyaraka za hati miliki ya gari kwa ajili ya kufanya biashara.

"Nilikwenda kuonana na Sabaya nikiwa nimebeba nyaraka za mkataba wa kumiliki gari na kadi ya gari kwa ajili ya kufanya biashara," alidai na kuongeza kuwa alipofika katika eneo hilo, alimkuta Sabaya akiwa na watu sita wakiwamo wanawake na wanaume.

Shahidi huyo alimtaja Nyegu kuwa mmoja wa watu waliokuwapo wakati wa kuuza gari hilo, kwa kumtambua kwa jila lake na wengine aliwatambua kwa kuwagusa mbega. Pia alidai kuwa Nyegu alijitambulisha kuwa ni msaidizi wa Sabaya.

Alidai kwamba baada ya nyaraka kukaguliwa na Sabaya aliomba akaunti namba yake na ya Filikunjombe kwa ajili ya kutuwekea fedha.

"Wakati tukiendelea na utaratibu wa kunilipa fedha za kuuziana gari, aliomba kuandikishiana mkataba na mimi badala ya Filikunjombe akidai kwamba anamtambua mimi tu na baada ya saa mbili walinitumia picha kwa whatsapp ikionyesha muamala wa Sh. milioni 39 umeingia kwa Filiku Njombe na alimpigia kuumuliza kama fedha imeingia katika akaunti yake na alithibitisha kupokea.

"Sabaya alikuja na fedha taslimu mkononi Sh. milioni 21, alinipatia mimi Sh. milioni 20 na milioni moja aliwapatia madalali," alidai na kubainisha kuwa alimuuzia Sabaya gari hilo kwa Sh. milioni 60 huku yeye akichukua Sh. milioni 20 na Filikunjombe Sh. milioni 40.

Hata hivyo, alidai kwamba baada ya kufanya biashara hiyo, alimwomba Sabaya kumpatia kijana wa kumsindikiza baada ya kupokea fedha hizo kwa kuwa mazingira hayakuwa rafiki.

"Kulikuwapo na watu ambao siwaelewi pia kulikuwa na silaha aina ya shotgun, hivyo nilipata hofu na ilinibidi kumwomba anipatie kijana wa kunisindikiza hadi katika biashara yangu kwa kuwa ndio ilikuwa sehemu sahihi ya kwenda na fedha hizo," alidai shahidi.

Shahidi huyo alionyeshwa nyaraka ya mkataba wa mauziano ya gari na aliiomba mahakama kupokea kama kielelezo cha ushahidi mahakamani.

Baada ya mawakili wa utetezi, wakiongozwa na Moses Mahuna kupitia nyaraka hizo, walikubali zipokewe kama kielelezo kwa kuwa hawakuwa na pingamizi.


EAST AFRICAN CRUDE OIL PIPELINE

**OMBI LA KUONYESHA NIA: UGAVI WA PEMBEJEO NA VIFAA KILIMO KWA MRADI WA EACOP.**
**KUMB: 0010007355.**

Total Energies East Africa Midstream B.V (Kampuni) Tanzania, Kampuni ya Kimataifa ya Mafuta na Gesi, inaalika taasisi zenye weledi na uzoefu kuonesha nia ya kutoa huduma ya kutekeleza programu ya Urejeshaji wa Ustawi wa Maisha kwa kaya zilizoguswa na Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP).

Mradi wa EACOP unahusisha ujenzi na uendeshaji wa bomba litakalofukiwa chini ya ardhi litakalovuka mipaka ya nchi mbili na litakalosafirisha mafuta kutoka eneo la Ziwa Albert nchini Uganda mpaka Pwani ya Mashariki ya Tanzania kwa ajili ya kusafirisha mafuta hayo kwenda katika masoko ya Kimataifa. Bomba hili litaanzia Kabaale katika wilaya ya Hoima nchini Uganda, mpaka Chongoleani, Mkoani Tanga nchini Tanzania. Urefu wa Bomba ni kilomita 1,443, kati ya hizo, kilomita 1,147 zitakuwa Tanzania, ambapo bomba hilo litapita kwenye mikoa nane (8) ambayo ni Kagera, Geita, Shinyanga, Tabora, Singida, Dodoma, Manyara, na Tanga; bomba la mafuta pia litapita kwenye Halmashauri za Wilaya 27 na vijiji 231.

**MAELEZO MAFUPI KUHUSU MAWANDA YA HUDUMA:**

Kampuni inahitaji mkuza wa ardhi pamoja na maeneo ya vituo kwa ajili ya ujenzi na uendeshaji wa shughuli za bomba la mafuta. Mchakato wa utwaaji wa ardhi umefanyika kwa kuzingatia sheria za nchi ya Tanzania pamoja na matakwa ya Mashirika ya Fedha ya Kimataifa. Utoaji wa ardhi mbadala ya kilimo na makazi kwa watu waliguswa na mradi (PAPs) na msaada wa Urejeshaji wa Ustawi wa Maisha vinatolewa kwa Kaya zilizoguswa na mradi.

Mradi unatafuta kampuni ya Kitanzania yenye weledi, uzoefu na uwezo wa kutoa huduma ya ugavi wa pembejeo na vitendea kazi vya kilimo katika ''Maeneo ya Kipaumbele'' yaliyopo kwenye mkuza wa bomba la mafuta ghafi. Wilaya ambako vitu hivyo vinapaswa kupelekwa ni:

**1.Kanda ya Magharibi:**
- Wilaya za Misenyi na Muleba (mkoa wa Kagera).
- Wilaya za Chato na Bukombe (mkoa wa Geita).

**2.Kanda ya Kati**
- Wilaya ya Kondoa (mkoa wa Dodoma).
- Wilaya ya Igunga (mkoa wa Tabora).
- Wilaya ya Iramba (mkoa wa Singida).

**3.Kanda ya Mashariki**
- Wilaya ya Kiteto (mkoa wa Manyara).
- Wilaya za Handeni na Muheza (mkoa wa Tanga).

Mawanda hii inahitaji ugavi wa pembejeo na vifaa vya kilimo vifutavyo ambavyo kiasi kinachohitajika kitabainishwa baadae:

(a) Mbegu za aina ya hybrid na/au OPV za mahindi, karanga, maharagwe n.k. zenye ubora wa hali ya juu.
(b) Miche ya mimea ya ndizi na mihogo.
(c) Mbolea ya chumvichumvi na chokaa ya kilimo.
(d) Madawa ya kilimo.
(e) Vifaa vya kilimo ikiwa ni pamoja na vipulizia dawa vya knapsack.
(f) Vifaa vazi vya usalama kazini ikiwa ni pamoja na suruali iliyoungana na shati(overall), viatu, miwani na maski.

Hifadhi ya vitu hivyo kabla ya kuvikabidhi utakuwa ni wajibu wa mkandarasi na vitakaguliwa na kufuatiliwa na wafanyakazi wa kampuni.

**VIGEZO MUHIMU VYA KUZINGATIA:**

Taasisi zitakazoonesha nia zinaalikwa kuambatanisha maombi yao pamoja na taarifa zifuatazo:

- Uthibitisho wa usajili kama shirika/taasisi ambayo shughuli zake zinahusiana moja kwa moja na ugavi wa pembejeo na vitendea kazi vya kilimo.
- Uthibitisho wa usajili wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) pamoja na cheti cha uthibitisho wa kulipa kodi kwa mwaka wa fedha uliopita.
- Maelezo mafupi kuhusu uzoefu na uwezo wa kufanya ugavi wa bidhaaa zinazohitajika.
- Inashauriwa, mwonyesha nia atume maombi ya kusajiliwa na kanzi data ya EWURA (LSSP) kama mtoaji na msambazaji wa huduma ndani ya nchi wakati wa kuwasilisha ombi la kuonesha nia ya kutekeleza shughuli za progamme.
- Inafuata Kanuni za Ushirikishwaji wa Watanzania, 2017 na ufafanuzi wa kampuni.

**KAMPUNI inaruhusu Wazabuni kuwasilisha pendekezo kwa ajili ya kanda mbili au zote tatu.**

Taasisi zenye nia ya kuleta maombi na ambazo zina uwezo na rasilimali za kutekeleza shughuli au kazi zilizoorodheshwa hapo juu yanapaswa kueleza nia yao pamoja na kuambatanisha pamoja na nyaraka zilizotajwa hapo juu kupitia barua pepe kwa **eacop-tz.eoi.1000001@totalenergies.com**(ukubwa wa barua pepe 20 Mb) saa au kabla ya**17:00** saa za Afrika Mashariki (EAT) tarehe **29th December 2021.**

**Angalizo:** Mradi wa EACOP utapitia na kuchambua nyaraka zilizotumwa na taasisi zitakazoonyesha nia ili kutengeneza orodha ya taasisi za awali zenye vigezo vinavyotakiwa. Taasisi zitakazokidhi vigezo tu ndiyo zitapokea na kusaini Makubaliano ya Utunzaji wa Taarifa (NDA) pamoja na mwaliko wa kuwasilisha zabuni katika kuendeleza mchakato wa zabuni. Maelezo yote ya kuonyesha nia yanapaswa kuandikwa kwa lugha ya Kiingereza.



Mkuu wa Mauzo Vodacom Kanda ya Dar es Salaam na Pwani, Brigita Shirima (kulia), akiwa na washindi wa promosheni ya "Show Love Tule Shangwe" ambao wamejishindia televisheni za kisasa, simu janja na safari kwenda kutalii, baada ya kukabidhiwa zawadi zao jijini Dar es Salaam jana. PICHA: **MPIGAPICHA WETU**

# Chanjo mbili mpya za corona kuja

**Na Waandishi Wetu**

WIZARA ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, imesema kufikia mwishoni mwa mwaka huu mpaka mwanzoni mwa mwaka ujao, inatarajia kupokea chanjo nyingine mpya mbili za ugonjwa wa corona.

Akizungumza katika mkutano wa wamiliki, wahariri na waandishi wa habari Dar es Salaam jana ulioandaliwa na Shirika la Umoja wa Mataifa linalohudumia Watoto (UNICEF) kwa kushirikiana na Jukwaa la Wahariri Tanzania (TEF), kuhusu umuhimu wa chanjo ya ugonjwa wa corona, Mkurugenzi wa Chanjo wa Wizara hiyo, Dk. Florian Tinuga, alisema kati ya hizo chanjo itakayoanza kuletwa kati ya hizo mbili ni Modema ndani ya mwezi au mwanzoni mwa Januari mwakani.

Alisema baada ya Modema, itakayofuata ni ya Sinovac ambayo na yenyewe italetwa nchini mwanzoni mwa mwaka ujao.

"Kwa hiyo mpaka mwanzoni mwa mwaka ujao tutakuwa tumeingiza aina tano za chanjo kati ya tisa ambazo zimethibitishwa na Shirika la Afya Duniani (WHO), kwa sababu mpaka sasa tumeingiza aina tatu tayari," alisema Dk. Tinuga.

**1,217,628 WACHANJA**

Dk. Tinuga alisema mpaka sasa idadi ya Watanzania waliokwisha kuchanja ni milioni 1,217,628 sawa na asilimia 2.11 na kwamba lengo la serikali ni kuchanja asilimia 60 ya Watanzania wote.

Alisema asilimia 80 ya wananchi wanaougua ugonjwa wa corona hawaendi hospitali, na kwamba wanaofika hospitalini baada ya ugonjwa huo ni asilimia 15 tu, huku asilimia tano pekee ndio hubainika kuugua na kuwa mahututi kisha kulazwa katika vitengo vya uangalizi maalum (ICU).

"Kwa hiyo bado kuna tatizo la wananchi kutokwenda kwenye vituo vya afya pale wanapougua ugonjwa huu, wengi wao wanaugulia nyumbani," alisema Dk. Tinuga.

Dk. Alex Mphuru kutoka UNICEF, alisema chanjo ya Pfizer imeshaanza kutumika kuchanja watoto katika baadhi ya nchi duniani, na kwamba bado utafiti mbalimbali unaendelea kwa ajili ya chanjo upande wa kundi la watoto.

Mtaalamu wa mawasiliano UNICEF, Usia Nkhoma, alisema bado kuna haja kwa vyombo vya habari kuendelea kutoa elimu juu ya umuhimu wa chanjo ya ugonjwa wa corona.

Mwenyekiti TEF, Deodatus Balile, alisema kama vyombo vya habari vitaendelea kutoa elimu kuhusu umuhimu wa chanjo ya ugonjwa huo.

Mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi (MUHAS), Prof. Deodatus Kakoko, alisema uvumi ulioenea juu ya athari za chanjo za UVIKO -19 kwa watakaochoma ulizorotesha kwa kiasi kikubwa kasi ya utoaji chanjo ilipoingia kwa mara ya kwanza nchini.

Alisema siku 43 za mwanzo walitoa chanjo 300,000 tu Tanzania nzima na hii ilitokana na imani potofu kuhusu chanjo hiyo na mwitikio ulianza kuwa mkubwa baada ya kutoa elimu kwa wananchi kuhusu usalama wa chanjo hizo.

Alisema baadhi ya uvumi ulioenea ni kuwa chanjo ya UVIKO inaathiri uzazi kwa wanawake na kuwafanya wasizae, inaathiri nguvu za kiume, imelenga kumaliza wa Afrika, inatoa taarifa za siri za mtu na kuwa waliougua COVID -19 hawana haja ya kupata chanjo hiyo.

Akitolea majibu ya uvumi huo, Prof. Kakoko alisema si kweli kwa kuwa hakuna ushahidi wowote wa kisayansi unaothibitisha ukweli wa uvumi huo na kuwa hata kama mtu aliugua ugonjwa huo anahitaji kupata chanjo kwa kuwa kazi yake ni kuweka na kuimarisha kinga za mwili.

Mpaka sasa Tanzania imeshapokea aina tatu za chanjo ya ugonjwa wa corona ikiwamo Johnson &Johnson, Pfizer na Sinopharm.

**Imeandikwa na Elizabeth Zaya na Jenifer Gilla.**

# Mapingamizi utetezi kesi ya Mbowe yagonga mwamba

**Na Kulwa Mzee**

MAHAKAMA Kuu Divisheni ya Makosa ya Rushwa na Uhujumu Uchumi, imetupilia mbali mapingamizi ya utetezi, hivyo kupokea maelezo ya onyo ya mshtakiwa wa tatu kuwa kielelezo cha Jamhuri katika kesi ya ugaidi inayomkabili Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Freeman Mbowe, na wenzake watatu.

Mahakama hiyo mbele ya Jaji Joackim Tiganga jana ilipokea kielelezo hicho cha maelezo ya mshtakiwa Mohammed Ling'wenya yaliyokuwa yanapingwa kupokewa baada ya ushahidi wa utetezi kukosa mashiko na nguvu.

Akisoma uamuzi huo, Jaji Tiganga alisema katika kesi ndogo upande wa Jamhuri ulikuwa na mashahidi wanne na upande wa utetezi mashahidi watatu.

Katika hoja ya kwanza kwamba mshtakiwa alikuwapo Kituo Kikuu cha Polisi Dar es Salaam, shahidi ASP Jumanne na Koplo Goodluck walidai walipotoka Moshi Agosti 5, 2020 wakifika kituoni hapo na jina la mshtakiwa limo katika kitabu cha kumbukumbu za mahabusu.

Alisema ushahidi unaonyesha mshtakiwa aliingizwa kituoni hapo na alitolewa kwa njia ya upelelezi.

Mshtakiwa wa tatu Ling'wenya anayedai alifikishwa Kituo cha Polisi TAZARA, alishindwa kuita mtu aliyemwona kituoni hapo kama shahidi badala yake alimwita shahidi wa tatu upande wa utetezi, Komandoo Gabriel Mhina, ambaye hakukutana naye TAZARA bali walikutana gerezani akamweleza alikuwa TAZARA.

Jaji alisema mahakama inaona ushahidi huo hauna nguvu.

Alisema ushahidi unatolewa kuhusu Mei 14, 2020 wakati jambo linalobishaniwa la Agosti 7, 2020 labda kama shahidi huyo alikuwa Oysterbay Agosti 7, 2020.

"Kwa mazingira hayo Mahakama inaona ushahidi wa shahidi huyo hauna thamani na hauwezi kuisaidia mahakama.

"Upande wa mashtaka ulieleza kuwa shahidi huyo alikuwa shahidi mwenye maslahi. Katika ushahidi wake alikuwa mwenye kujikanganya hasa pale alipodai alimwelekeza Koplo Msemwa akamchukulie fedha zake alizokabidhi Oysterbay Polisi wakati katika ushahidi anadai alipokamatwa hakuwa na fedha.

"Mahakama inatilia shaka ushahidi wake, ushahidi wa upande wa utetezi unatakiwa kutengeneza mashaka, hautakiwi wenyewe kutiliwa shaka, ni shahidi mwenye maslahi. Alisema haridhiki kuanzia kesi mpaka kwa jaji mwenyewe. Mahakama inaona ni shahidi wa hisia ambaye amekuja mahakamani kutoa hisia zake," alisema Jaji Tiganga akizungumzia shahidi wa utetezi, Lembrus Mchome.

Alisema mahakama inaona ushahidi uliotolewa na upande wa mashtaka haujatikiswa kwa sababu hiyo pingamizi namba moja kwamba mshtakiwa Ling'wenya hakuwapo Kituo Kikuu cha Polisi Dar es Salaam, linatupiliwa mbali si la msingi.

Jaji pia alisema hoja kwamba mshtakiwa wa tatu aliteswa, alilazimishwa kutia saini maelezo kwa kutishwa na ASP Jumanne, upande wa Jamhuri unadai hakuteswa, askari walipowatoa Kituo cha Polisi cha Kati Agosti 8, 2020 kuwapeleka Mbweni hawajurudi.

"Mahakama inabakia njia panda ni lini mshtakiwa aliteswa. Hoja za mawakili wa utetezi zinaonyesha aliteswa Agosti 9, 2020 na maelezo alichukuliwa siku hiyo hiyo wakati Jamhuri wanadai alichukuliwa maelezo Agosti 7.

"Mahakama imeshindwa kujua ni tarehe ipi mshtakiwa aliteswa, kwa sababu hiyo Mahakama inabakia na mkanganyiko," alisema Jaji Tiganga.

Alisema pingamizi kwamba maelezo yalichukuliwa nje ya muda halina mashiko, sheria inaelekeza kwamba muda hautahesabiwa kama mshtakiwa atasafirishwa na uzito wa kesi yenyewe.

Kwa mujibu wa Jaji, hakuna ubishi kwamba mshtakiwa alikamatwa Moshi Agosti 7, 2020, walikamatwa wawili badala ya watatu, walichukuliwa na kufikishwa Dar es Salaam Agosti 7, mwaka huo.

"Pingamizi hili naona halina mashiko. Mahakama inaona kwa mazingira hayo maelezo yalichukuliwa Dar es Salaam ilikuwa sahihi," alisisitiza Jaji.

Mahakama hiyo iliyatupilia mbali mapingamizi yote saba na kupokea maelezo ya onyo, inasema yalichukuliwa kwa utaratibu.

Washtakiwa katika kesi hiyo mbali na Mbowe na Ling'wenya ni Adamu Kasekwa, na Halfani Bwire ambao wanakabiliwa na mashtaka sita ya kula njama kufanya ugaidi kati ya Mei Mosi na Agosti 5, 2020.

## HABARI KITAIFA



Wananchi wakipita kwa tabu kutokana na madimbwi ya maji yaliyoko katika Mtaa wa Kasanga, eneo la Gerezani Kariakoo, jijini Dar es Salaam jana, ambapo wafanyabiashara wa eneo hilo wameitaka mamlaka kukarabati barabara hiyo kwani imekuwa kikwazo kwa wateja kuingia kwenye maduka yao. **PICHA: MARY GEOFREY**

# Waziri Mabula: Kubalini mabadiliko mipango ardhi

**Na Munir Shemweta,** MUFINDI

SERIKALI imewataka wananchi wanaoishi maeneo yanayofanyiwa mipango ya matumizi bora ya rdhi kukubaliana na mabadiliko katika maeneo yao ili kuepuka athari zinazoweza kutokea ikiwamo uharibifu wa mazingira kwenye vyanzo vya maji.

Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, alisema hayo jana alipokuwa akizungumza na wakazi wa kijiji cha Idetelo, Mufindi wilayani Iringa.

Dk. Mabula aliwaomba wananchi kuzingatia utaratibu waliojiwekea kwa kuwa mpango huo unaainisha maeneo kwa ajili ya shughuli mbalimbali kama vile kilimo, ufugaji na huduma za jamii na tofauti yoyote ya utekelezaji wake, itasababisha athari kubwa zikiwamo za kimazingira.

Aliwaelezea wakazi wa Idetelo wanaofanya shughuli za kilimo katika ukingo wa chanzo cha maji cha Mpogolo kuwa wana wajibu wa kuhakikisha mpango huo unazingatiwa kwa kuwa chanzo hicho ni muhimu kutokana na kupeleka maji mto Ruaha unaopeleka maji kwenye mradi mkubwa wa umeme wa bwawa la Mwalimu Nyerere.

"Niwaombe mzingatie huu mpango wa matumizi bora ya ardhi ulioletwa kwa kuwa utaepusha athari ya uharibifu wa mazingira. Wazee wangu ninyi ni mashahidi Idetelo iliyokuwa miaka ya nyuma ni tofauti kabisa na ya sasa," alisema.

Wananchi wa kijiji hicho kupitia mkutano na Naibu Waziri, pamoja na kukubaliana na uamuzi wa serikali wa kuacha kufanya shughuli za kilimo kwenye ukingo wa chanzo cha maji cha Mpogolo, waliiomba serikali kuwatafutia njia mbadala itakayowawezesha kujipatia kipato kuendesha maisha yao kwa kuwa mategemeo yao yalikuwa chanzo hicho.

Dk. Mabula alishauri upangaji mipango ya matumizi bora ya ardhi uzingatie mahitaji ili kuepuka migogoro na kubainisha kuwa eneo la hekta 40 zilizotengwa kwa ajili ya shughuli za ufugaji katika kijiji ni ndogo na hali hiyo inaweza kuzua migogoro kati ya wakulima na wafugaji.

"Hapa wafugaji ni wengi lakini maeneo machache, hivyo tunatakiwa kuwashauri wafugaji namna bora ya ufugaji ikiwamo 'zero grazing' (ufugaji usio wa kuhamahama) na wakulima tuwashauri kilimo kisichoharibu ikolojia," alisema.

Pia alizitaka halmashauri zote nchini zenye mipango ya matumizi bora ya ardhi kuhakikisha mipango hiyo inasimamiwa pamoja na kutenga fedha za utekelezaji wake sambamba na kutoa elimu kwa wananchi ili mpango ufahamike na kutekelezwa kwa ufasaha.

Mkuu wa Wilaya ya Mufindi, Saadi Mtambule, alisema mpango wa matumizi bora ya ardhi katika wilaya hiyo utapunguza migogoro ya ardhi katika eneo hilo na kusisitiza kuwa wilaya hiyo haitakuwa sehemu ya kukwamisha mradi huo.

# Kicheko wagonjwa wa kwanza kupandikizwa uloto Muhimbili

**Na Romana Mallya**

WAGONJWA watano waliopandikizwa uloto katika Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH) tawi la Mloganzila, wameruhusiwa kutoka hospitalini hapo baada ya kupatiwa matibabu kwa siku 17.

Mkurugenzi Mtendaji wa MNH, Prof. Lawrence Museru, aliwaambia waandishi wa habari jana kuwa huduma hiyo ya upandikizaji uloto imefanyika kwa mara ya kwanza na kwa mafanikio makubwa.

Alisema wagonjwa hao ambao wanatoka Dar es Salaam, Njombe, Mara na Zanzibar, matibabu yao yamekwenda vizuri na sasa wanawaruhusu kwenda nyumbani.

"Tunashukuru matibabu ya wagonjwa hawa yamekwenda vizuri na kawaida matibabu yake au mchakato mzima unachukua kati ya siku 14 mpaka siku 30. Wagonjwa wetu hawa wametumia siku 17 na wote wanaendelea vizuri na leo (jana) au kesho (leo) wataruhusiwa kutoka hospitalini," alisema.

Prof. Museru alisema kwa sasa hospitali hiyo kupitia serikali inajipanga kujenga jengo maalumu Mloganzila litakalotumika kwa ajili ya kupandikiza uloto, figo na magonjwa mengine kama hayo.

Mmoja wa wagonjwa hao, Fadhil Mdagano, kutoka Njombe, aliishukuru serikali kwa kuwezesha kupatikana kwa huduma hiyo hapa nchini.

"Sisi wote tuliopata huduma hii tunaendelea vizuri. Tunawashukuru sana madaktari na wafanyakazi wa hospitali kwa huduma nzuri. Tumekuwa wagonjwa wa kwanza kupata huduma hii na kwa kweli imeturejeshea furaha, tunaendelea vizuri," alisema Mdagano.

Daktari Bingwa wa Magonjwa ya Damu Muhimbili, Dk. Stella Rwezaura, aliwashukuru wagonjwa hao kwa kukubali kupata huduma hiyo hospitalini hapo.

"Hii ni huduma ya kwanza na hawa wagonjwa watano ni wa kwanza kufanyiwa matibabu haya, kwa kuangalia ugeni wa huduma hii, tunawashukuru sana wao na ndugu zao kwa kukubali kufanyiwa huduma hii," alisema.

Tanzania imeandika historia nyingine kwenye utoaji huduma bobezi katika nchi zilizopo Ukanda wa Afrika Mashariki na Kati kwa kuanzisha huduma ya upandikizaji uloto (bone marrow transplant) inakuwa nchi ya kwanza Afrika Mashariki na Kati na ni moja ya nchi sita pekee Afrika zinazotoa huduma hiyo.

Aina hiyo ya matibabu inahusisha uvunaji, uchakataji na upandikizaji (urejeshaji) wa chembe-hai mama (stem cells) za damu na hutolewa kwa watu wenye magonjwa ya saratani za damu (leukemia, multiple myeloma, saratani inayohusisha matezi-lymphoma). Hutolewa pia kwa wagonjwa wasioweza kuzalisha chembe-hai za damu kama aplastic anaemia pamoja na wagonjwa wa selimundu (siko seli) na thalassemia.

Serikali mwaka jana ilitoa Sh. bilioni saba ili kuwezesha uanzishwaji wa huduma hiyo ikiwa ni pamoja na ujenzi wa kituo cha umahiri katika upandikizaji. Sehemu ya fedha hizo zimewezesha kununua vifaa na kusomesha wataalamu.

# Polisi lawamani kwa kumwachia mtuhumiwa

**Na Faustine Feliciane**

JESHI la Polisi wilaya ya Kahama mkoani Shinyanga limelalamikiwa na mfanyabiashara Rehema Mwagao wa mkoani humo kwa madai ya kumwachia anayetuhumiwa kutapeli dola 25,847.5 (Sh. milioni 48.6).

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Mwagao alidai mtuhumiwa huyo ni mkazi wa Dar es Salaamu na mmiliki wa kampuni inayojihusisha na mikopo.

Alidai kuwa mtuhumiwa alikamatwa na polisi Mei mwaka huu na kupelekwa kituo cha polisi Kahama, akidaiwa kujipatia fedha kwa njia ya udanganyifu kisha kuachiwa kwa dhamana katika mazingira yenye utata.

Mfanyabiashara huyo alisema makubaliano yao yalikuwa ni kupatiwa mkopo wa mashine za kukoboa mpunga kutoka kampuni ya India ambayo aliunganishwa nayo ili kupata mkopo wa riba nafuu.

"Baada ya makubaliano alitaka nimlipe kiasi cha pesa dola 25,847.50 ambazo ni sawa na Sh. milioni 48.6 kwa thamani ya mwaka 2016. Nilimwingizia pesa hizo kwenye akaunti namba ... (anataja namba) ya CRDB kwa awamu mbili tofauti," alidai mfanyabiashara huyo.

Hata hivyo baada ya kutapeliwa alimsaka mtuhumiwa na kufanikiwa kumpeleka kituo cha polisi lakini akashangaa mtuhumiwa akabadilishiwa tuhuma kutoka utapeli na kufunguliwa kesi ya madai.

Kamanda Polisi Mkoa wa Shinyanga, George Kyando, alikiri kuwa na taarifa za sula hilo na kwamba mama huyo alifikisha malalamiko yake ofisini kwake na alisikilizwa na kuchukuliwa maelezo.

"Baadaye Jeshi la Polisi tulipoona kuna utata tuliomba msaada wa kisheria kwenye Ofisi ya Mwendesha Mashtaka wa Kahama na ndipo tulipojibiwa kuwa imekuwa kesi ya madai na sio kesi ya jinai kama anavyoisema mlalamikaji," alisema Kamanda Kyando.

Mwendesha Mashtaka wa mkoa wa Shinyanga, Magreth Ndaweka, alidai bado hajaliona faili la kesi hiyo kwa kuwa halijafika ofisini kwake, hivyo hawezi kulizungumzia na kumtaka mwandishi kumtafuta Mwendesha Mashtaka wa wilaya ya Kahama.

Mwendesha Mashtaka wa wilaya, Mercy Ngowi, alikiri kulifahamu shauri hilo lakini hakutaka kuelezea kwa kina kwa maelezo kwamba hana mamlaka ya kulizungumzia.


Victoria FINANCE

Victoria Finance Plc
5th Floor, Sky Tower Building-Kijitonyama
New Bagamoyo Road
P.O. Box 12102, Dar es Salaam - Tanzania
Telephone +255 22 277 4577
Fax: +255 22 277 4559
Email: info@victoriafinance.co.tz
Website: www.victoriafinance.co.tz

**TANGAZO LA MINADA YA HADHARA**

**VICTORIA FINANCE PLC** INAPENDA KUUTANGAZIA UMMA WA WATANZANIA YA KWAMBA KWA IDHINI ITAKAYOTOA KWA KAMPUNI TOFAUTI ZA UDALALI INATARAJIA KUUZA KWA MNADA WA HADHARA DHAMANA ZA WADAIWA SUGU KAMA IFUATAVYO;

| NA | JINA LA MDAIWA | DHAMANA | AINA NA SEHEMU YA DHAMANA | DALALI | TAREHE |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | CRISPIN FRANCIS OCHANDA | NYUMBA | MKATABA WA MAUZIANO- MAPINGA BAGAMOYO | JODAC PROFESSINALS LTD | 30-12-2021 |
| 2 | JELEMIA LIHO | NYUMBA | MKATABA WA MAUZIANO- MAJENGO MADIBIRA | PAMOJA AUCTION MART | 31-12-2021 |
| 3 | DANIEL NDELE | PAGALA | MKATABA WA MAUZIANO- MAGUNGULI MAHANGO MADIBIRA | PAMOJA AUCTION MART | 31-12-2021 |
| 4 | HURUMA KIMKANGA | NYUMBA | MKATABA WA MAUZIANO- MAGUNGULI MAHANGO MADIBIRA | PAMOJA AUCTION MART | 31-12-2021 |
| 5 | MAGDALENA MATEI | NYUMBA | MKATABA WA MAUZIANO- KABETE MADIBIRA | PAMOJA AUCTION MART | 31-12-2021 |
| 6 | SAMWEL M. BONENKA | GARI | MAZDA T 219 DGP | UMOJA PROFESSINALS LTD | 30-12-2021 |
| 7 | TITUS BEDA AZIMIO | GARI | TOYOTA HARRIER T 508 BXF | UMOJA PROFESSINALS LTD | 30-12-2021 |

Minada yote itafanyika mahali husika katika muda na siku ambayo itatangazwa kupitia katika vipeperushi na magari ya matangazo kutokana na idhini itayotoka kutoka katika ofisi za wanaohusika.

**MASHARTI YA MNADA;**

- Asilimia 25% ya bei iliyofikia italipwa papo hapo na asilimia 75% iliyosalia ilipwe ndani ya siku kumi na nne. (14). Kwa kushindwa kufanya hivyo itapelekea mnada kurudiwa tena na pesa zilizolipwa kutokurudishwa.
- Gharama za kumuhamisha mmiliki na kubadili umiliki ni juu ya mnunuzi.
- Dhamana itauzwa Kama ilivyo.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Utoroshaji wa madini udhibitiwe kuepusha upoteaji wa mapato

**RAIS** Samia Suluhu Hassan, juzi alisema bado kuna utoroshaji wa madini, hivyo kuzitaka mamlaka zote kushirikiana kudhibiti hali hiyo, ambayo inalitia hasara taifa.

Moja ya jitihada za udhibiti ni kujenga ukuta eneo la Mererani mkoani Manyara, ili kuepusha uchepushaji wa madini aina ya tanzanite ambayo pekee hupatikana nchini, lakini biashara hiyo ilifanyika nchi jirani na kufifisha ukweli wa upatikanaji wa rasilimali hiyo.

Nyingine ni kujenga masoko ya madini kwenye mikoa mbalimbali hasa yenye uzalishaji wa rasilimali hiyo ambayo yameonyesha mafanikio makubwa ikiwamo halmashauri kupata kodi ya huduma.

Aidha, uwapo wa masoko hayo iliboresha bei ya madini na katika kila kilichouzwa kiliuzwa kwa njia halali na kuiwezesha nchi kupata mapato sahihi na kwa wakati tofauti na awali ambayo ilifanyika kwa kificho.

Mwaka 2017 Bunge lilifanya mabadiliko ya Sheria ya Madini ya mwaka 2010 ambayo iliongeza malipo ya mrabaha kutoka asilimia nne hadi sita kwa madini ya metali yakiwamo dhahabu, shaba na fedha. Pia, iliongeza malipo ya mrabaha kutoka asilimia tano hadi sita kwa madini ya vito yakiwamo rubi, garnets na tanzanite.

Mbinu nyingi za udhibiti zilifanyika kwenye marekebisho ya Sheria ya Fedha na Sheria ya Kodi ambayo inataka kila kampuni au mtu anayetaka kusafirisha madini nje ya nchi, madini yake yatakaguliwa na kuthaminishwa na atalipa ada ya ukaguzi ambayo ni asilimia moja ya thamani ya madini anayosafirisha.

Kutokana na sheria hiyo, mchimbaji mdogo anayeuza madini kwa wanunuzi wa kati au wanunuzi wakubwa atakatwa asilimia tano ya thamani ya madini na kupelekwa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA).

Pia kwenye mipaka kumekuwa na udhibiti kuhakikisha madini hayatoki kiholela nchini bali Watanzania wanaona manufaa kupitia kodi mbalimbali ambazo huingia kwenye kuhudumia huduma za kijamii.

Kauli ya Rais kuwa utoroshaji bado upo maana yake mamlaka zinazohusika hazijatekeleza wajibu wake sawasawa kusimamia na kulinda rasilimali hiyo isitoroshwe, hivyo kuathiri masoko yaliyojengwa, hivyo serikali kukosa mapato.


Tayari vyombo vya dola vimeagizwa kufuatilia kwa karibu ili kudhibiti wanaofanya hivyo, na tunatarajia kuona hatua zaidi zinachukuliwa na inawekwa wazi waliohusika na kilichofanyika kukomesha hali hiyo.

Ni lazima hatua zichukuliwe haraka ili kuepusha Tanzania kuwa shamba la bibi kwamba kila mtu anaweza kujichotea rasilimali awezavyo na kutoweka nazo pasipo kujulikana.

Bila udhibiti wa rasilimali hiyo nchi itaendelea kupoteza zaidi, hivyo ni lazima kukomesha mtandao wa utoroshaji ikiwamo kurudisha nguvu ya udhibiti iliyofanyika kipindi cha nyuma na kuwafikisha mahakamani wote wanaohusika ili iwe fundisho kwa wengine.

Kuacha mianya hiyo ni kuwakatisha tamaa wale wanaolipa kodi stahiki, huku wengine wakijinufaisha kwa njia za panya ambazo zinaumiza wengi.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Kupenda uvumi, uongo kunavyoangusha wengi

Na Jenifer Gilla

**UVUMI** ulioenea juu ya athari mbaya za chanjo za COVID-19 kwa watakaochanjwa, unaelezwa kuwa umezorotesha kasi ya upokeaji wa chanjo ilipoingizwa nchini kwa mara ya kwanza,

Mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi za Afya (MUHAS), Profesa Deodatus Kakoko, anaeleza.

Kwa mara ya kwanza dozi 1,000,000 za chanjo ya Johnson & Johnson kutoka Marekani ziliingizwa nchini na kukutana na upinzani kutoka kwa viongozi wa dini pamoja na wanasiasa, waliokuwa wanadai ni mpango wa Wazungu kuangamiza Waafrika.

Akizungumza katika mkutano wa chanjo ya UVIKO -19 uliokutanisha wataalamu wa afya na wanahabari ukiandaliwa na Jukwaa la Wahariri (TEF) jijini Dar es Salaam, mtaalamu huyo anaeleza kuwa siku 43 za mwanzo walitoa chanjo 300,000 pekee kwa Tanzania nzima.

Anaongeza kuwa hali hiyo ilitokana na imani potofu kuhusu chanjo hiyo kwa madai kuwa watu watapata athari nyingi, lakini mwitikio ulianza kuwa mkubwa baada ya kutoa elimu kwa wananchi kuhusu usalama wa chanjo hizo.

Anakumbusha baadhi ya uvumi ulioenea ni kuwa chanjo ya UVIKO-19 inaathiri uzazi kwa wanawake na kuwafanya wagumba, inaathiri nguvu za kiume, imelenga kumaliza Waafrika, inatoa taarifa za siri za mtu na kuwa waliougua COVID -19 hawana haja ya kupata chanjo hiyo.

Profesa Kakoko anasema madai hayo ni uvumi usio na ukweli kwa kuwa hakuna ushahidi wa kisayansi unaothibitisha maelezo hayo na kwamba hata kama mtu aliugua ugonjwa huo anahitaji kupata chanjo kwa kuwa kazi yake ni kuweka na kuimarisha kinga za mwili.

Anasema wajawazito wanachoma chanjo, lakini wagonjwa wa maradhi sugu kama presha, sukari na saratani wanapata chanjo.

Anashauri watoto wasubiri kwanza, kwa mujibu wa daktari bingwa wa watoto kutoka Shirika la Kimataifa la Kutetea Haki za Watoto (UNICEF), Dk. Alex Mphuru. Japo nchi nyingine zimeruhusu watoto kuanzia miaka 12 kupata chanjo ya corona aina ya pfizer kwa Tanzania hajjaruhusu kwa sababu bado haijajiridhisha na usalama wa chanjo hiyo.

Kwa mujibu wa wataalamu hao kinachoonekana ni Watanzania kuwa na tatizo la kusikiliza na kukumbatia masuala ya uongo kuliko ukweli wa mambo. Kwa mfano kuna baadhi ya watu wanapinga matumizi ya vyandarua vyenye dawa kwa maelezo kuwa vinahatarisha afya wakidai vinasababisha ugumba na vina sumu inayoua polepole.

Si hivyo tu kuna baadhi ya kinamama na familia nyingine zinazoamini kuwa watoto wenye degedege hawatakiwi kutibiwa hospitalini bali kwa waganga wa kienyeji.

Tena kuna watu wanaoamini kuwa maziwa ya mama ya mwanzo ni uchafu yanamdhuru mtoto. Licha ya kampeni kufanyika kila mwaka na kuhimizwa kuwanyonyesha watoto baada ya kujifungua, kuna wengine wanaoamini kuwa yanatakiwa kukamuliwa ukutani kwanza hadi yawe meupe ili kuepusha athari kwa watoto.

Ni vyema sasa watu kuamka na kuujua ukweli kuwa, taarifa za kitafiti na kitaalamu ni muhimu kuliko hizo za kuokoteza mitaani ili kuachana na mienendo ya kupenda kusikiliza zaidi uongo, uvumi na masuala ya upotoshaji yasiyowajenga.

Imani potofu kuwa ugonjwa wa UVIKO- 19 unawapata wazee pekee na wadhaifu nayo ni changamoto iliyosababisha vijana kupuuza tahadhari na kuishi kienyeji pengine hata kusambaza COVID-19.

Ni wakati wa kuachana na mienendo isiyo na tija na pale wanapoona kuna upungufu, Watanzania wajifunze kufuata wataalamu na kuujua ukweli na kuepuka hadaa, maana madhara yanaweza kuwa makubwa hata kuangamia.

## Polepole, Bulembo wakosolewa

**Na Sabato Kasika**

MAKADA wa CCM, Humphrey Polepole na Abdalah Bulembo wametakiwa kutumia njia sahihi kukosoana badala ya vyombo vya habari na majukwaa yasiyo rasmi, kwa kuwa ni kinyume cha utaratibu.

Wamekumbushwa kuwa chama kina utaratibu wake wa kushughulikia malalamiko ya wanachama ikiwa ni pamoja na kupeleka katika vikao vya ngazi mbalimbali kuanzia tawi si mwingine zaidi ya huo.

Ushauri huo ulitolewa jana na kada wa CCM na Mwenyekiti Mtendaji wa Taasisi ya Utawala Bora na Maendeleo Tanzania CEGODETA, Thomas Ngawaiya, alipozungumza na gazeti hili Dar es Salaam, jana.

Ngawaiya alikuwa akizungumzia hatua ya Bulembo kumsema Polepole kwa kutumia vyombo vya habari badala kushawishi vikao vya chama kumwita ili kumhoji kauli zake za kuisema serikali.

"Yaani ni kwamba, wote wamekosea. Polepole anatumia jukwaa lisilo rasmi kuisema serikali halafu Bulembo naye anajitokeza kujibu bila kufuata utaratibu ambao ni vikao vya chama," alisema Ngawaiya.

Alisema chama hakina utaratibu wa kuitisha vyombo vya kusuluhisha, na kuwataka makada hao kutambua kuwa hayo ni malumbano ambayo yanaweza kuwakanganya wananchi.

"Wote wanaweza kuwa na nia njema, lakini sisi watu wa utawala bora tunaona kwamba, njia walizotumia si sahihi, kwani haipendezi kumkosoa kiongozi wa nchi kwa kutumia jukwaa lisilo rasmi na pia si sahihi kukosoana kwa kutumia vyombo vya habari," alisema.

Pia aliishauri serikali na vyombo vyake vya dola kutumia sheria kuzuia mambo kama hayo yaishie pale Bulembo alipomkosoa Polepole na kwamba yasipewe nafasi ya kuwachanganya wananchi.

Wiki iliyopita, Bulembo ambaye amewahi kuwa Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wazazi ya CCM, alikaririwa na vyombo vya habari akimtaka Polepole amwache Rais Samia Suluhu Hassan atekeleze majukumu yake.

Alikuwa akimjibu Polepole kuhusu lawama zake dhidi ya Rais Samia ambaye ni mwenyekiti wa CCM, huku akisisitiza kuwa anakemea suala hilo kama mwanachama wa kawaida na hajatumwa na mtu.

Bulembo pia alimwomba makamu mwenyekiti wa chama hicho bara, Philip Mangula kumhoji Polepole kama alivyowahoji makatibu wakuu wa zamani, Abdulrahman Kinana na Yusuf Makamba.

# Waziri aruhusu usafirishaji wa gundi nje ya nchi

**Na Mwandishi Wetu,** ARUSHA

WAZIRI wa Maliasili na Utalii, Dk. Damas Ndumbaro, ameruhusu kusafirishwa nje ya nchi makontena 93 ya gundi (utomvu), sawa na tani 1,683 iliyokuwa imeshavunwa wakati akitoa tamko la kuzuia usafirishaji wa malighafi hiyo.

Dk. Ndumbaro alitoa ruksa hiyo jana jijini hapa baada ya kupokea ushauri kutoka kwa kamati ya kumshauri waziri kuhusu masuala ya misitu kabla ya kufanya mkutano wa wadau wa mazao ya misitu.

Kamati hiyo ilimshauri waziri kuwa gundi hiyo ambayo imekwishavunwa inapozidi kukaa inapoteza ubora wake, hivyo kutokufaa tena kwa matumizi. Kutokana na ushauri huo, alisema ameruhusu kusafirishwa kwa tani hizo ili gundi hiyo isiharibike pamoja na kuepusha hasara ambayo ingewapata wamiliki pamoja na serikali kukosa mapato.

"Hii gundi ni kemikali, inavyozidi kukaa inabadilika rangi na wataalamu wameniambia kuwa ikiendelea tu kukaa muda wake unaisha wa matumizi," alisema.

Gundi ni aina ya utomvu unaogemwa kwenye miti ya kupandwa aina ya misindano na malighafi hiyo husafirishwa kwenda nchi za nje lakini hadi hivi sasa, matumizi yake bado hayajafahamika kuwa inatumiwa kwa ajili ya kutengenezea vitu gani.

Hatua hiyo inakuja kutokana na agizo la kusitishwa kuvunwa na kusafirishwa kwa malighafi hiyo kwenda nje ya nchi alilolitoa Oktoba, mwaka huu akiwa mkoani Iringa baada ya kushindwa kupata maelezo ya kutosha kuhusiana na bei ya gundi hiyo pamoja na matumizi yake. Gundi hiyo ilikuwa ikisafirishwa kwenda nje ya nchi hususani China

Katika hatua nyingine, Dk. Ndumbaro ameendelea kushikilia msimamo wake wa kusitisha kuvuna utomvu huo hadi Chuo cha Sokoine cha Kilimo (SUA) na Taasisi ya Utafiti wa Misitu Tanzania (TAFORI) zitakapotoa utafiti ambao kwa sasa bado haujakamilika juu ya athari ya miti inayovunwa gundi hiyo.

Akifafanua katazo hilo, Dk. Ndumbaro alisema lina manufaa makubwa kwa Watanzania kwa ajili ya kutengeneza ajira nyingi kwa wananchi

"Baada ya kukamilika kwa ripoti kutoka TAFORI na SUA na kujiridhisha kuwa uvunaji hauna madhara, wafanyabiashara mtatakiwa kujenga viwanda hapa nchini na si habari ya kusafirisha," alisisitiza.




Meneja wa Benki ya NMB Tawi la Kiomboi, David Diwi (kulia), akikabidhi pikipiki ya magurudumu matatu kwa Joseph Kuttikkatt George, baada ya kuibuka mshindi katika droo ya NMB Bonge la Mpango Tumerudi Tena, katika Halmashauri ya Wilaya ya Kiomboi, mkoani Singida jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# TAKUKURU yatinga gerezani kutoa elimu

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

MKUU wa Dawati la Elimu kwa Umma wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Pwani, Fredrick Mbigili, amesema vitendo vya rushwa vikifumbiwa macho vinaweza kusababisha madhara kwa jamii ikiwamo umaskini na hata maradhi.

Mbigili aliyasema hayo juzi wakati watumishi wa taasisi hiyo walipotembelea gereza la Mkuza lililoko Kibaha na kutoa elimu kwa wafungwa na mahabusu.

Alisema wamefika katika gereza hilo kutoa elimu ili kuongeza uelewa wa sheria na athari zinazopatikana kutokana na vitendo vya rushwa kuanzia ngazi ya jamii hadi taifa.

Aliwataka wafungwa na mahabusu kuwa mabalozi wazuri wa kupinga rushwa pindi watakaporejea uraiani ili kuunga mkono juhudi za serikali kuhusiana na mapambano dhidi ya rushwa nchini.

Mkuu wa Gereza la Mkuza, George Osindi, aliishukuru TAKUKURU kwa kuratibu mpango huo wa elimu, akisema utawasaidia wafungwa na mahabusu kujenga hofu dhidi ya vitendo vya rushwa na kuwa raia wema pindi watakaporejea uraiani.

Aliwaomba wadau mbalimbali ikiwamo mashirika mbalimbali kujitokeza kutoa msaada wao wa hali na mali kwa wafungwa kwa kuwa wengi wao wanatoka nje ya mkoa, hivyo wamekuwa wakihitaji msaada wa mahitaji mbalimbali ikiwamo dawa za meno na sabuni. TAKUKURU Mkoa wa Pwani walitembelea gereza hilo na kutoa elimu ya mapambano ya rushwa kwa wafungwa na mahabusu ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya Siku ya Maadili Duniani.

# Waziri apongeza kampuni usalama wafanyakazi

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu, Jenister Mhagama, amekipongeza Kiwanda cha KIOO Limited kwa kuweka vifaa vya kisasa kwa ajili ya kuwahakikishia usalama wafanyakazi wake.

Aliyasema hayo juzi alipotembelea kiwanda hicho kuangalia kinavyojali sheria na kanuni za usalama pahala pakazi kama sehemu ya maadhimisho ya miaka 60 ya Uhuru.

Waziri Mhagama alisema kwa maelezo ya viongozi wa kiwanda hicho ameridhika kwa namna wanavyowajali wafanyakazi kwa kuhakikishia usalama wanapokuwa kazini. Kadhalika, Mhagama alisema amefurahi kuona namna maslahi ya wafanyakazi wa kiwanda hicho yanavyozingatiwa na namna kiwanda kinavyolipa kodi kubwa kiwa serikali.

"Kwa maelezo niliyopewa nimefurahi sana kuona mnazingatia maslahi ya wafanyakazi wenu na namna mnavyowahakikishia usalama wakiwa kazini endeleeni hivyo na wengine wahakikishe wanazingatia usalama," alisema.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Afya na Usalama Kazini (OSHA), Khadija Mwenda, naye alipongeza kiwanda hicho kwa kuwawekea mazingira mazuri wafanyakazi wake yanayowahakikishia usalama. Alisema viwanda vyote nchini vinapaswa kuweka mifumo bora ya kiusalama kama KIOO Limited ili kuhakikisha wafanyakazi wao wanakuwa salama muda wote wanapokuwa kazini. Meneja Rasilimali Watu wa Kiwanda hicho, Jacob Msuya aliishukuru serikali kupitia OSHA ambavyo imekuwa ikitoa miongozo mbalimbali ya namna ya kuweka mifumo ya kiusalama kiwandani hapo.

Msuya alisema menejimenti ya KIOO Limited imekuwa ikifanya linalowezekana kuhakikisha wafanyakazi wote wanakuwa salama wanapotekeleza majukumu yao.

Kioo Limited ni mzalishaji mkubwa wa chupa Afrika Mashariki na imewekeza vya kutosha ikiwa na wafanyakazi zaidi ya 600 wenye ajira za kudumu na vibarua kwenye idara mbalimbali.

Kwa sasa kiwanda hicho kina uwezo wa kuzalisha tani 400 za chupa kwa siku na kimekuwa kikiuza asilimia 60 ya bidhaa hiyo nje ya nchi baada ya kukidhi soko la ndani.




Meneja Biashara wa Kampuni ya Tigo, Suleiman Bushagama, akizungumza na waandishi wa habari wakati wa uzinduzi wa simu mpya ya Infinix Hot 11, jijini Dar es Salaam jana. Kulia ni Ofisa Uhusiano wa kampuni ya Infinix Tanzania, Aisha Karupa. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Habari za ushirika zaingizwa EJAT

**Na Marco Maduhu,** TANGA

BARAZA la Habari Tanzania (MCT) limeongeza kundi la habari za ushirika ambalo litashindaniwa mwakani kwenye Tuzo za Umahiri za Uandishi wa Habari Tanzania (EJAT) ambazo hutolewa na baraza hilo.

Ofisa Programu kutoka baraza hilo la habari, Paul Malimbo, alibainisha hayo jana kwenye mafunzo ya waandishi wa habari yaliyofanyika jijini Tanga kuhusu namna ya kuandika habari bora ambazo zitakuwa zikishindanishwa kwenye tuzo hizo za EJAT.

Mafunzo hayo yamefadhiliwa na Taasisi ya Utawala wa Maliasili (Natural Resources Governance Institute). Alisema baraza hilo limeongeza kundi la habari za ushirika ambazo zitaanza kushindaniwa mwakani kufuatia ombi la Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC) kuingiza kundi hilo kwenye kinyang'anyiro cha EJAT.

"MCT katika utoaji wa tuzo za EJAT mwakani, tumeongeza kundi la habari za ushirika, ambapo wakati wa mashindano litatazamwa katika vigezo vilevile vinavyotumika kwenye makundi mengine ambayo yanashindaniwa.

"Baada ya kuongeza kundi hili la habari za ushirika, hivyo kutafanya makundi yanayoshindaniwa kwenye Tuzo za EJAT kufika 19, ambapo makundi mengine ni: Habari za uchumi, biashara, fedha, michezo na utamaduni, kilimo, elimu, utalii na uhifadhi, uchunguzi, data, haki za binadamu na utawala bora, jinsia na watoto.

"Habari za gesi, mafuta na madini, walemavu, afya, sayansi na teknolojia, hedhi salama, mpigapicha bora, mchora katuni bora na kundi la wazi.

Mrajisi Msaidizi wa Vyama vya Ushirika mkoani Tanga, Henjewele John, alisema waliomba kundi hilo kuingizwa kuwaniwa katika tuzo hizo ili kutangaza kazi za ushirika na kuongeza chachu ya kutoa huduma kwa wakulima na kuwainua kiuchumi.

Alisema vyama vya ushirika vina mchango mkubwa nchini katika kuinua uchumi wa mkulima na kuongeza mapato ya serikali.

# Serikali kuendeleza uwekezaji wa elimu

**Na Benny Mwaipaja,** DUBAI

SERIKALI ya Tanzania imeihakikishia Jumuiya ya Kimataifa kwamba itaendelea kuwekeza rasilimali fedha kwa ajili ya kuendeleza elimu ili kuwa na jamii iliyoelimika kwa ajili ya maendeleo ya nchi.

Ahadi hiyo imetolewa mjini Dubai na Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Lameck Nchemba, kwenye kilele cha mkutano unaohusu uwekezaji kwenye sekta ya elimu katika karne ya 21 hasa baada ya janga la ugonjwa wa UVIKO-19 kuzitikisa nchi nyingi duniani.

Dk. Nchemba amesema kuwa Serikali itaendelea kuongeza bajeti ya sekta ya elimu kila mwaka kadri rasilimali fedha inavyopatikana na kuiomba jumuiya ya kimataifa kuchangia juhudi hizo za serikali.

Alisema kipaumbele cha serikali ni kuhakikisha kuwa kila mtoto anayetakiwa kwenda shule anapata elimu bila vikwazo kwa kutoa elimu bila malipo huku akiboresha mazingira ya shule nchini kote.

"Mheshimiwa Rais Samia ameelekeza pia fedha zilizotolewa na Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) zitumike ipasavyo na zitaleta mapinduzi makubwa katika elimu nasi tumewahakikishia wadau wa maendeleo fedha watakazotupatia zitatumika kwa malengo yaliyokusudiwa" alisema Dk. Nchemba.

Kwa upande wake, Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia Prof. Joyce Ndalichako, alisema kuwa Tanzania kuna utashi wa kisiasa wa kuendeleza elimu ambapo bajeti ya elimu imekuwa ikiongezeka kila mwaka na mpaka sasa imefikia zaidi ya asilimia 17 na kwamba huenda siku zijazo ikafikia asilimi 20 ya bajeti yote ya serikali.

Mkutano wa masuala ya elimu ujulikanao kama WirED umewashirikisha wadau mbalimbali kutoka duniani kote ambapo hoja mbalimbali za kuboresha elimu, ikiwemo kuwawezesha vijana, na kuimarisha masuala ya teknolojia yamejadiliwa kwa kina katika mkutano huo.

**Alisema kipaumbele cha serikali ni kuhakikisha kuwa kila mtoto anayetakiwa kwenda shule anapata elimu bila vikwazo kwa kutoa elimu bila malipo huku akiboresha mazingira ya shule nchini kote.**

# Benki ya Kilimo yapata Baraza la Wafanyakazi

**Na Mwandishi Wetu**

IKIWA ni sehemu ya utekelezaji wa Sheria ya Ajira na Uhusiano Kazini na Sheria ya Majadiliano ya pamoja katika Utumishi wa Umma, Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB) imefanya uchaguzi, kuunda Baraza la Wafanyakazi na kulizindua.

Akitoa elimu kabla ya uundaji wa Baraza Ofisa Elimu Kazi kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge, Vijana, Ajira na wenye Ulemavu Kamishna wa Kazi, Tulia Msemwa, alisema Baraza la Wafanyakazi ni jukwaa muhimu mahala pa kazi kwa kuwa ni kiunganishi kati ya Menejimenti na Wafanyakazi na lina mchango mkubwa katika kuleta ufanisi. Alibainisha kuwa baraza linajukumu la kuhakikisha wafanyakazi wanafahamu haki zao na wanatimiza wajibu wao kwa mujibu wa sheria na taratibu za utumishi wa umma.

"Uundwaji wa Baraza la Kazi hapa TADB utasaidia kuleta ufanisi kwa taasisi na taifa kwa ujumla. Ikumbukwe kuwa serikali inazingatia sana suala la taasisi zake kuwa na mabaraza ya wafanyakazi kwani yanaanzishwa kisheria kwa madhumuni ya kuishauri serikali katika ngazi za idara, taasisi na wizara kuhusu usimamizi wa kazi na rasilimali watu," alisema.

Akizungumza wakati wa kusimamia uchaguzi, Mwakilishi wa Chama cha Wafanyakazi Viwanda, Biashara, Taasisi za Fedha, Huduma na Ushauri (TUICO), Willy Kibona, alipongeza uongozi wa TADB kwa kuamua kuharakisha ukamilishaji wa uundaji wa Baraza la Wafanyakazi. Aliendelea kupongeza TADB kwa kushirikisha vyombo vya habari katika mchakato mzima. "Hii ni hatua kubwa na niombe taasisi nyingine ziweze kujifunza hapa. Suala la uundwaji wa mabaraza ya wafanyakazi linapaswa kufanyika kwa uwazi. Kipekee niseme kuwa ni mara ya kwanza kuona vyombo vya habari vikishirikishwa katika mchakato kama huu," alisema Kibona.

Mkurugenzi Mtendaji wa TADB, Frank Nyabundege, alisema kuwapo na uwakilishi kamilifu wa baraza la wafanyakazi kutasaidia kushauri na kuondoa viashiria vyovyote vya ubaguzi au uonevu katika eneo la kazi na kuongeza ari pamoja na ufanisi zaidi katika utendaji kazi.

"Kuundwa kwa baraza hili muhimu kutasaidi sana kuwa na njia nzuri na inayokubalika kisheria ya ushirikishwaji wa wafanyakazi na kuwezesha majadiliano yenye tija kwa taasisi yetu na kwa wafanyakazi wake. Pia litasaidia kuweka namna nzuri ya kuboresha mazingira ya kazi kwa kuzingatia sheria na taratibu zote katika kujumuisha wafanyakazi katika maamuzi na mipango ya taasisi yetu kuanzia sasa na kuendelea. Nia yetu ni kuona kuwa TADB inakuwa sehemu salama na yenye kufurahiwa kufanya kazi," alisema.

Wafanyakazi wa TADB walipata elimu kabla ya zoezi la uchaguzi wa wakilishi kutoka kila idara na uwakilishi kutoka kanda zote. Zoezi hili lilikamilishwa na Mkurugenzi Mtendaji ambaye ni mwenyekiti wa baraza kwa kukata utepe mkataba baina ya Taasisi na Chama cha Wafanyakazi kuashiria kuanza kazi rasmi kwa baraza hilo.

# UNHCR yatoa msaada wa maji shuleni

**Na Deogratius Nsokolo,**
KIBONDO

SHIRIKA la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Wakimbizi (UNHCR) limekabidhi miradi ya maji na usafi wa mazingira katika Shule ya Msingi Kibondo wilayani Kibondo mkoani Kigoma.

Mwakilishi wa mkuu wa shirika hilo wilayani Kibondo, Frolinus Mukiza, amesama wakati wa kukabidhi msaada huo kuwa mpango wa UNHCR kusaidia jamii inayozunguka kambi za wakimbizi ni utaratibu endelevu ili kusaidia utatuzi wa changamoto mbalimbali.

Mukiza alisema pamoja na jukumu la kulinda wakimbizi, msaada huo unalenga kusaidia maendeleo katika maeneo yanayoathiriwa na ujio wa wakimbizi kwa kutekeleza kwa kushirikiana na serikali kutekeleza miradi mbalimbali na hasa katika sekta ya elimu, afya na maji.

Alisema mradi wa ujenzi wa vyoo vya kisasa katika Shule ya Msingi Kibondo utasaidia wanafunzi kusoma vizuri baada ya kumaliza tatizo hilo ambalo limekuwa likisababisha wanafunzi kwenda kujisaidia nyumba za jirani na shule hiyo.

Watekelezaji wa mradi huo UNHCR la nchini na Norway kupitia kwa mratibu wake, Violet Bipyuye, ambaye alisema mradi huo ambao umegharimu zaidi ya shilingi milioni 60, umewezesha kujenga vyoo vya kisasa vya walimu na wanafunzi, kuweka mfumo wa maji na kutoa vifaa vya usafi.

Alisema katika mradi kuna vyoo maalum kwa ajili ya walemavu na chumba maalum kwa ajili ya mahitaji maalum kwa wanafunzi wasichana hasa wakiwa katika siku za hedhi.

Naye mwalim mkuu wa shule hiyo, Slanus Ezbon, alisema msaada huo unairejesha shule hiyo katika ustaarabu kwa kuwa watoto sasa wataweza kusoma muda wote.

"Shule hii ina wanafunzi zaidi ya 1,800, ilikuwa na hali mbaya kutokana na uhaba wa vyoo, lakini sasa tatizo limekwisha," alisema Ezbon.

Ofisa elimu ya msingi wilayani Kibondo, Jamhuri Kidumu, alisema wilaya hiyo bado inakabiliwa na kikwazo kikubwa katika miundombinu ya shule za msingi na hasa vyoo bora na huduma ya maji ambapo alitoa wito kwa wazazi na wananchi kushirikiana na shule kutatua vikwazo hivyo.

Akizungumza baada ya kupokea msaada huo, Katibu Tawala wa Wilaya ya Kibondo, Ayoub Sebabili, alisema serikali itaendelea kushirikiana na mashirika ya ndani na nje katika utatuzi wa vikwazo mbalimbali vinavyowakabili wananchi.




Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB), Frank Nyabundege (wapili kulia), akikabidhi mkataba wa kuunda Baraza la Wafanyakazi kwa ofisa kutoka Ofisi ya Kamishna wa Kazi, Tulia Msemwa, baada ya kumalizika kwa uchaguzi wa baraza hilo, jijini Dar es Salaam jana. Kulia ni Katibu Mkuu aliyechaguliwa, Edna Nyatta na Katibu Mkuu Msaidizi, Abdi Jangawe Msuya. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Waitwa TBS kupata alama ya ubora

**Na Mwandishi Wetu,**
MWANZA

WAJASIRIAMALI wameshauriwa kujitokeza kwa wingi kupata alama ya ubora inayotolewa na Shirika la Viwango Tanzania (TBS), hatua ambayo itawasaidia kuwaondolewa vikwazo vya kibiashara kwenye ukanda wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC).

Wito huo ulitolewa kwa nyakati tofauti na Ofisa Masoko wa TBS, Rhoda Mayugu, wakati akizungumza na wajasiriamali walioshiriki Maonyesho ya 21 ya Nguvu Kazi Jua Kali ya Afrika Mashariki ambayo yaliyomalizika Jumapili jijini Mwanza.

Maonyesho hayo yaliyoanza Desemba 2, mwaka huu, yalihudhuriwa na washiriki kutoka nchi sita za Sudan Kusini, Tanzania, Burundi, Kenya Rwanda na Uganda.

"Wajasiriamali ambao hawajapata alama ya ubora wahakikishe bidhaa zao zinathibitishwa na TBS, kwani wakishakuwa na alama hiyo hawapati kikwazo chochote kwenye masoko ya nchi za EAC, wanapita mipakani pasipokuwa na kikwazo chochote," alisema Mayugu na kuongeza:

"Kwa faida hiyo wanayoipata tunawashauri wengine ambao wameshiriki maonyesho haya ambao bidhaa zao hazijapata alama ya ubora wahakikishe zinathibitishwa na TBS kwa sababu Jumuiya ya Afrika Mashariki inatambua alama ya ubora ya nchi husika."

Alifafanua kwamba hatua hiyo inawaongezea wigo wa masoko, hivyo ni muhimu wale ambao hajathibitisha bidhaa zao wazithibitishe.

Alisema miongoni mwa majukumu ya TBS ni kutoa elimu kwa wazalishaji pamoja na wafanyakazi wa sekta na taasisi za viwanda kuhusiana na uzalishaji wa bidhaa bora, uzalishaji salama na udhibiti wa ubora.

"Kwa hiyo katika kutimiza lengo hilo kwenye maonyesho haya tunawaelimisha wajasiriamali kuhusiana na alama ya ubora.Wanatakiwa kujua kwamba bidhaa zote ambazo zimethibitishwa ubora wake ambazo zinazalishwa nchini na zimethibitishwa ubora wake huwa zinatumia alama ya ubora.

"Hii alama ya ubora inakuwa na manufaa kwa pande zote mbili, upande wa mzalishaji, mfanyabiashara na kwa mtumiaji."

Alisema kwa upande wa wafanyabiashara na wazalishaji wakiwamo wajasiriamali alama ya ubora inawapa nguvu na kujiamini kwamba bidhaa zao zinakidhi viwango vya bidhaa husika katika nchi yetu.

Kwa upande wa watumiaji, Mayugu alisema alama ya ubora inawafanya wawe na uhakika kwamba bidhaa hiyo imekaguliwa na haina madhara kwa matumizi ya bidhaa husika, hivyo inamhakikishia kwamba bidhaa hiyo inakidhi viwango vya kitaifa. "Kwa hiyo mtumiaji anakuwa na uhakika kwamba hiyo bidhaa nikiitumia siwezi kupata madhara yoyote," alisema Mayugu.

# Waziri Mkumbo awapa siri w/biashara bidhaa za sikukuu

Na Christina Mwakangale

WAZIRI wa Viwanda na Biashara, Prof. Kitila Mkumbo, ametoa wito kwa wafanyabiashara wa bidhaa zinazoendana na msimu wa sikukuu za Krismasi na Mwaka Mpya, kuwa wabuni na kuziuza kwa bei nafuu.

Amesema nchi zilizoendelea wafanyabiashara hutumia fursa na soko kubwa la wanunuzi hususan mwishoni mwa mwaka kwa kuuza bidhaa ikiwamo nguo kwa bei nafuu.

Akizungumza jana mkoani Dar es Salaam, Prof. Kitila wakati akifungua duka la LC Waikiki ambalo ni kwa ajili ya mauzo ya bidhaa za nguo na viatu eneo la Mlimani City, alisema wafanyabiashara nchini waige utamaduni wa nchi zilizoendelea kulitumia vyema soko la mwisho wa mwaka.

"Wafanyabiashara nchini wapunguze bei za bidhaa zinazohitajika mwishoni mwa mwaka kwa sababu uhakika wa kuuza ni mkubwa ili kila Mtanzania anufaike na sikukuu. Sio inapoonekana mahitaji yanaongezeka bei wanaongeza, wenzetu kila mwisho wa mwaka wanapunguza mauzo," alisema Prof. Mkumbo.

Alisema duka hilo limetoa ajira za moja kwa moja kwa Watanzania 50 na kwamba Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), itakusanya kodi kupitia biashara hiyo, hivyo nchi kukuza uchumi wake.

Meneja Masoko wa duka hilo, Micky Decha, alisema bidhaa zinazouzwa dukani hapo zina ubora unaokubalika kwa kuwa zinatengenezwa kwa pamba kwa kiwango cha asilimia 100.



Katibu Tawala wa Mkoa wa Kagera, Prof. Faustine Kamuzora (katikati), sambamba na Mkurugenzi wa Wateja Binafsi wa Benki ya NBC, Elibariki Masuke, (wapili kushoto), wakishiriki katika uzinduzi wa bweni jipya kwa ajili ya wanafunzi wa kike wa Shule ya Sekondari ya Tunamkumbuka, benki hiyo imetoa msaada wa vitanda 60 kwa ajili ya wanafunzi hao. Wengine ni Mkuu wa Shule hiyo, Robert Muganyizi (kushoto), wazazi na wanafunzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# NBC yapiga jeki shule ya wasichana vitanda

Na Mwandishi Wetu

BENKI ya NBC imetoa msaada wa vitanda 60 kwa ajili ya wanafunzi wa Shule ya Sekondari ya Tunamkumbuka iliyoko wilayani Bukoba mkoani Kagera.

Msaada huo ni hatua ya benki hiyo kuunga mkono jitihada za shule hiyo kuwasaidia wanafunzi wa kike kuondokana na adha ya kutembea umbali mrefu baada ya kukamilisha ujenzi wa bweni la wasichana la shule hiyo.

Akizungumza kwenye hafla fupi ya uzinduzi wa bweni hilo uliokwenda sambamba na makabidhiano ya vitanda hivyo iliyofanyika shuleni hapo mapema wiki hii, Mkurugenzi wa Wateja Binafsi wa Benki ya NBC, Elibariki Masuke, alisema vitanda hivyo vyenye thamani ya Sh. milioni 14 vitatumika katika bweni hilo litakalokuwa na uwezo wa kuchukua wanafunzi mia moja na ishirini.

"NBC tuliguswa na jitihada zilizoonyeshwa tayari na wadau mbalimbali katika kufanikisha ujenzi wa bweni hili wakiwamo wananchi wenyewe na serikali na hivyo kwa kutambua umuhimu wa elimu iliyo salama kwa mtoto wa kike tukaona ni vema tusaidie kufanikisha hili watoto wetu wasome katika mazingira salama zaidi," alisema.

Kwa upande wake Katibu Tawala wa Mkoa wa Kagera, Prof. Faustine Kamuzora, pamoja na kuishukuru benki hiyo kwa msaada huo, pia aliiomba kuweka msukumo katika ufundishaji wa somo la fedha na matumizi yake katika shule za sekondari ili kuwajengea msingi wa nidhamu ya fedha tangu wakiwa wadogo.

"Kwa kuwa mitaala yetu haizungumzii sana masuala ya elimu ya fedha kwa wanafunzi ni vema taasisi za kifedha zinazoguswa na masuala ya elimu kama ilivyo Benki ya NBC kuangalia namna ya kusaidia katika kutoa mafunzo kwa wanafunzi wakiwa wadogo ili waweze kuanza kuelewa nidhamu ya fedha na matumizi yake wakiwa wadogo," alisema.

Naye Mkuu wa Shule hiyo, Robert Muganyizi, alisema ujenzi wa bweni hilo uliombatana na msaada wa vitanda vilivyotolewa na Benki ya NBC utasaidia sana wanafunzi hao ambao hapo awali walikuwa hawapati muda wa kujisomea kutokana na uchovu waliokuwa wanaupata kutokana na wao kutumia muda mwingi kutembea kurudi na kwenda hapo huku wakihatarisha usalama wao nyakati za usiku.

"Kuzinduliwa kwa bweni hili kutawaweka katika mazingira bora kitaaluma tofauti na ilivyokuwa mwanzo ambapo walikuwa wakilazimika kutembea zaidi ya kilometa thelathini na mbili ili kufika shuleni wakiwa wamechoka na hivyo kuzorotesha hata jitihada zao kimasomo. Tunashukuru sana wadau wote waliojitokeza kufanikisha hili ikiwamo Benki ya NBC kwa msaada wao wa vitanda," alisema.

Aidha, ujenzi wa bweni la wanafunzi wa kike katika Shule ya Sekondari Tunamkumbuka umegharimu zaidi ya shilingi milioni 63 ambapo NBC imechangia shilingi milioni 14, Mfuko wa Maendeleo Tanzania TDT ukichangia shilingi milioni 32 huku jamii ikichangia zaidi ya shilingi milioni 16.

## Skauti wanawake wapata viongozi

Na Sabato Kasika

CHAMA cha Skauti wa Kike Tanzania (TGGA), kimechagua viongozi wapya ambao wataongoza chama hicho kwa kipindi cha miaka mitatu ijayo.

Baadhi ya viongozi hao ni Kamishna Mkuu, Mary Richard, Mwenyekiti wa chama, Consolata Shayo, Mwenyekiti wa Vijana, Irene Jeremiah na Katibu wa Vijana, Unisiata Makoko.

Uchaguzi wa viongozi hao ulifanyika jijini Dar es Salaam jana na kuhudhuriwa na watu wa kada mbalimbali akiwamo Waziri wa zamani wa Fedha, Zakia Meghji, Meja Jenerali mstaafu, Zawadi Madawili na wengine.

Akizungumza katika uchaguzi huo, Makamu Mwenyekiti wa Bodi ya chama hicho, Victoria Mandali, aliwataka viongozi wapya kuendeleza pale wenzao walipomaliza muda wao walipoishia.

"Uongozi ni mamlaka au karama ya kuwaonyesha watu njia kwa vitendo, ili kufika malengo tarajiwa, kwa hiyo nanyi fanyeni hivyo kwa kushirikiana na wale mnaowaongoza na kuweka maono yatakayowezesha kufika malengo, maendeleo tarajiwa,"alisema Mnadali.

Alisema ni muhimu wawe waadilifu, wanyenyekevu, kwa kuwa kiongozi ni mtu anayeongoza njia, ili kufikia jambo tarajiwa, na kwamba wawe na uwezo wa kushawishi kuwavuta wengine ili wawafuate.

"Wanachama wana matarajio makubwa kwenu, hivyo kwa miaka mitatu ijayo mtafanya kile ambacho ni matarajio yao kwa maendeleo ya chama, nasi bodi tunawatakia majukumu mema," alisema.

Kamishna mpya wa chama hicho, Mary Richard, aliwashukuru wanachama wenzake kwa kuwa na imani naye, huku akiahidi kutowaangusha na kwamba atafanya kazi kwa kufuata katiba ya chama hicho.

"Binafsi sina mengi ya kuongea, ila ninawaahidi kwamba sitawaangusha, nitafanya kazi kwa karibu nanyi, katiba ya chama chetu ndiyo itaniongoza kutekeleza majukumu yangu," alisema Mary.

Kabla ya uchaguzi huo, chama hicho kilikuwa kikiongozwa na Symphorosa Hangi (Kamishna Mkuu) na Prof. Martha Qorro (Mwenyekiti), ambao pamoja na viongozi wengine, wamemaliza muda wao wa miaka mitatu.

KUIMARISHA ULINZI MITAANI
Wadau: Ziundwe nyumba 10 ndani ya serikali za mitaa
Ukurasa 12





Ukurasa 14

Uhuru anapomkubali Raila uchaguzi 2022



MZOZO WA MAKOMREDI CCM

# Wadau wakitumia chama ujumbe kijilinde, kikemee

**Na Sabato Kasika**

SAKATA la makada wa CCM, Humphrey Polepole na Abdalah Bulembo, kukosoana hadharani, limewaibua baadhi ya wadau wa siasa, ambao wametoa maoni kuhusu kuzozana kwa makomredi hao waliohudumu awamu ya tano.

Mchambuzi wa siasa Said Msonga, akizungumzia mzozo huo, anashauri CCM kulinda hadhi yake kwa kuzuia malumbano kati ya wanachama wanaoibuka na kukosoa viongozi hadharani au wenyewe kwa wenyewe kuzozana.

Anasema, uwajibikaji wa pamoja, ni wa muhimu hasa wanachama wanapoambiana au kukosoana kupitia majukwaa ya chama ili kulinda taswira ya chama mbele ya umma wa Watanzania.

"Kama mwanachama ana hoja ya msingi kuna nafasi na sehemu ya kuipeleka, ila kwa tafsiri ya kawaida ni kwamba, mtu anapotoka hadharani na kukosoa viongozi wa chama au wa serikali hawasaidii bali anaongeza mpasuko," anasema Msonga.

Anaeleza kuwa , kutumia majukwaa ya ndani, husaidia viongozi kufanya kazi zao kikamilifu, kwa kuwa ndiyo wanaobeba mawazo na maono ya umma kupitia njia hizo na siyo kama mbinu inayotumiwa na wanachama hao.

"Chama kikongwe kama CCM, makada wake walipaswa kutambua hilo na siyo mmoja kusokoa serikali hadharani na mwingine 'kumshambulia' mwenzake kwa maneno kupitia vyombo vya habari," anasema.



Abdallah Bulembo, Mwenyekiti mstaafu wa Jumuiya ya Wazazi ya CCM. **PICHA: MTANDAO**

Mchambuzi huyo anahoji kulikuwa na haja gani kuwaambia Watanzania kuwa Polepole alipewa shati la chama na Nape Nnauye?

Na kwamba chama kinatakiwa kutengeneza nidhamu kwa kuchukua hatua mapema, ili iweje?

"Kinachozungumzwa na Polepole katika darasa lake la uongozi ni kizuri, lakini njia anayotumia ndiyo ambayo haionyeshi uwajibikaji wa pamoja, inaweza kuchukuliwa kama utovu wa nidhamu," anasema.

**WOTE WAMEKOSEA**

Kada mwenzao wa CCM na Mwenyekiti Mtendaji wa Taasisi ya Utawala Bora na Maendeleo Tanzania (CEGODETA) Thomas Ngawaiya, anawakosoa kuwa walichofanya hakifurahishi.

Ngawaiya anasema, wanatakiwa kutumia njia sahihi kukosoana badala ya majukwaa yasiyo rasmi au vyombo vya habari na kwamba hatua hiyo ni kinyume na taratibu za chama hicho kikongwe.

"Nikiwa kiongozi wa taasisi inayojishughulisha na utawala bora, lakini pia kada wa CCM, ninawakumbusha kutumia utaratibu wa chama wa kushughulikia malalamiko ya wanachama," anasema Ngawaiya.

Anataja baadhi ya taratibu hizo kuwa ni kupeleka malalamiko au hoja katika vikao mbalimbali vya chama, kuanzia ngazi ya tawi hadi taifa na siyo kulalamikia kwingine au kujibizana kwenye vyombo vya habari.

Anasema, hata kama Polepole ana hoja, hapaswi kutumia jukwaa lisilo rasmi kuisema serikali, na Bulembo naye anajitokeza kujibu bila kufuata utaratibu ambao ni vikao vya chama, na kwamba wote wana makosa.

"Wote wanaweza kuwa na nia njema, lakini sisi watu wa utawala bora tunaona njia walizotumia si sahihi, kwani haipendezi kumkosoa kiongozi wa nchi kwa kutumia jukwaa lisilo rasmi na pia si sahihi kuzozana kwa kutumia vyombo vya habari," anasema Ngawaiya.

Anaongeza kuwa pamoja na kwamba ana asasi ya utawala bora, hawezi kuitumia kusema au kuikosoa serikali hadharani, badala yake atafuata njia sahihi kufikisha ujumbe wa taasisi hiyo mahali husika.

Kwenye sakata hili, ninaishauri serikali na vyombo vyake vya dola kutumia sheria kuzuia mambo kama hayo yaishie pale Bulembo alipomkosoa Polepole, yasipewe nafasi ya kuwachanganya wananchi.

**NYUMA YA PAZIA**

Mkurugenzi wa Jukwaa la Katiba Tanzania (JUKATA) Bob Wangwe, anasema, suala hilo lina mambo mengi yamejificha nyuma ya pazia, ikiwamo watu kutaka mamlaka za uteuzi ziwaone na pia kuzuia uhuru wa wengine kutoa maoni.

Anaongeza kuwa siyo hapo tu bali hata 'darasa la Polepole' kwenye mitandao ni matokeo ya kuwapo kwa makundi ya watu ambayo yameundwa ndani ya uongozi na mbunge huyo wa kuteuliwa anaweza kuwa miongoni mwa watu wanaochukuliwa kama waliokuwa kwenye ngazi za juu," anasema Wangwe.

Anafafanua kuwa kitendo cha kushushwa daraja ndicho kimesababisha hayo yote anayoyafanya na kwamba wapo wanaomshangilia na wengine kumkosoa hadharani, na kwamba kila mmoja ana mwelekeo na mtizamo wake.

"Wale wanaomshangilia ndiyo waliokuwa wakifaidika na mfumo uliopita na wengine wanaomkosoa hadharani ni wale ambao wanataka uongozi wa sasa uwaone na kuwapa nafasi au wanaukumbusha uwakumbuke."

Mkurugenzi huyo anasema, kinachotakiwa kufanywa na Watanzania kwa sasa ni kujadili maendeleo yao na ya nchi kwa ujumla badala ya kuzungumzia masuala ya watu au kushambuliana kwa maneno hadharani kwa kutaka kufurahisha uongozi.

Mkwaruzano wa wawili hao ulianza wiki iliyopita, baada ya Bulembo Mwenyekiti wa zamani wa Jumuiya ya Wazazi CCM, alikaririwa na vyombo vya habari akimtaka Polepole amwache Rais Samia Suluhu Hassan atekeleze majukumu yake.

Alikuwa akimjibu Polepole kuhusu lawama zake dhidi ya serikali na Rais ambaye ni Mwenyekiti wa CCM, huku akisisitiza kuwa anakemea suala hilo kama mwanachama wa kawaida na hajatumwa na mtu.

Bulembo pia alimuomba Makamu Mwenyekiti wa CCM Bara, Philip Mangula kumhoji Polepole kama alivyowahoji waliokuwa Makatibu Wakuu wa CCM, Abdulrahman Kinana na Yusuf Makamba na kuchukua hatua.



Kada wa CCM na Waziri mstaafu Stephen Wasira. **PICHA: MTANDAO**

KUIMARISHA ULINZI MITAANI

# Wadau: Ziundwe nyumba 10 ndani ya serikali za mitaa

**Na Sabato Kasika**

AMANI, umoja na mshikamano ni tunu za Watanzania tangu uhuru mwaka 1961 ambazo wanaziendeleza hata sasa katika shughuli za kila siku.

Ushirikiano huo hautoki mbinguni bali unalindwa na kutunzwa , ndiyo maana katika jitihada za kuhakikisha nchi inaendelea kuwa ya amani na utulivu, CCM inataka kamati za ulinzi na usalama katika wilaya na mikoa ziwatumie mabalozi wa nyumba kumi kutambua wahalifu na wahamiaji haramu wanaoingia nchini kutishia amani na usalama katika maeneo yao.

Hatua hiyo inaelezwa kuwa itafanikisha mpango huo kwa kuwa mabalozi hao kupitia vikao vyao vya mashina wanaweza kusaidia katika kupata taarifa sahihi na kupanga mipango ya maendeleo ya wilaya na mikoa, kwa kuwa wanakuwa na taarifa za idadi ya watu wakazi katika mashina yao.

Katibu Mkuu wa CCM Daniel Chongolo, anataka watumike, kwa kuwa wao wana taarifa za kutosha kuhusu wahusika halali wa maeneo yao na wageni kuanzia ngazi ya mashina hadi wilaya.

Chongolo alitoa maelekezo hayo katika ziara ya hivi karibuni ya kukagua uhai wa chama mkoani Kigoma alipozungumza na wanaCCM wa shina namba sita la kata ya Nyamidaho wilaya ya Kasulu.

Ni baada ya Mkuu wa wilaya ya Kasulu Kanali Isaac Mwakisu, kueleza uwepo wa mamia ya wahamiaji haramu kutoka Burundi katika wilaya hiyo wanaojihusisha na shughuli mbalimbali ikiwamo vibarua kwenye mashamba ya wenyeji (Watanzania) ndani ya wilaya hiyo.

Kufuatia hatua ya CCM kukumbushia mabalozi wa nyumba kumi kwenye suala la amani na utulivu, Nipashe inazungumza na kada mbalimbali kupata maoni yao kuhusu umuhimu wao katika ulinzi na usalama zama hizi za vyama vingi.

### KUANGALIA NYUMA

Mkurugenzi Mtendaji mstaafu wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), cha Dar es Salaam, Dk. Hellen Kijo-Bisimba, anasema mfumo wa mabalozi wa nyumba kumi ulikuwa kiungo muhimu cha umoja na mshikamo wakati wa uongozi wa chama kimoja.

Anasema, baada ya mfumo wa vyama vingi nyumba 10 ziliachwa japo zilikuwa zinafanya kazi kwa karibu zaidi na wananchi kama ilivyokuwa hapo awali.

"Nyumba kumi zilikuwa ni chache ambazo balozi anaweza kuzimudu kuzungukia, tofauti na sasa kuna wajumbe wa serikali za vitongoji, vijiji na mitaa ambao wanaongoza eneo kubwa," anasema Kijo-Bisimba.

Anafafanua kuwa katika kitongoji, kijiji au mitaa kuna nyumba nyingi ambazo si rahisi wajumbe kuzifikia na kujua nini kinaendelea, na kwamba ni muhimu kutazama upya makosa hayo na kuyafanyia kazi.

"Kwa sasa tunatakiwa kuwa na wajumbe wa nyumba kumi wanaotokana na serikali za vitongoji, vijiji au mitaa badala ya kuwaacha wakifanya kazi katika maeneo makubwa wasiyoyamudu," anasema.

Anashauri ndani ya mfumo huo maeneo yagawanywe ili kuwapata wajumbe na nyumba zao 10 kufanikisha ulinzi na usalama , kwa vile wote watakuwa wanafahamiana.

Anaongeza kuwa ulinzi wa amani unatakiwa uanzie katika nyumba kumi wanaotokana na serikali, badala ya kuwarundikia nyumba nyingi .

### MWAMKO MDOGO

Mchambuzi wa siasa, Gwandumi Mwakatobe, anasema, baada ya kuingia kwenye mfumo wa vyama vingi, majukumu yaliyokuwa yakifanywa na wajumbe hao, sasa yapo kwa wajumbe wa serikali za vitongoji, vijiji na mitaa.

Anasema, wajumbe wa serikali za vitongoji, vijiji na mitaa, wanatakiwa kujua idadi ya maeneo yao, wageni na hata wale wanaojihusisha na vitendo vya uvunjifu wa amani na kutoa taarifa kwa uongozi wa serikali ya eneo husika.

"Tatizo ni kwamba mwamko wa baadhi ya wajumbe ni mdogo, siyo kama enzi ya zamani ya wajumbe wa nyumba kumi, wakati huo chama kimeshika hatamu, viongozi wa juu walifuatilia kwa karibu," anasema Gwandumi.

Anasema, hata sasa mtu anapotaka kuhama sehemu moja kwenda nyingine, anatakiwa kuwa na barua kutoka kwenye serikali ya kitongoji, kijiji au mtaa ambayo inamtambulisha kule anakokwenda.

Mchambuzi huyo anasema, baadhi ya watu hawafuati utaratibu huo na pia hata viongozi wa ngazi hiyo hawafuatilii, na kwamba hali kama hiyo inaweza kuchangia kuwapo kwa wahamiaji haramu na vitendo vya uhalifu.

"Lakini pia baadhi ya Watanzania wenyewe hata wakiona kuna wahalifu kwenye maeneo yao, hawatoi taarifa kwenye serikali, badala yake hadi wawe na shida zao ndipo utawaona kwenye ofisi za serikali," anasema.

### MAZINGIRA SI RAFIKI

Mkongwe wa siasa na waziri mstaafu, Steven Wasira, anasema, utaratibu wa kutumia wajumbe wa nyumba kumi kwenye ulinzi na usalama ulikuwa mzuri, ila kwa sasa mazingira hayaruhusu tena.

"Lakini mazingira ya sasa hayaruhusu, baada ya kuwapo kwa mfumo wa vyama vingi, mabalozi wa nyumba kumi wamebaki kuwa viongozi wa chama kwenye makazi yao," anasema Wasira.

Anasema, serikali haikuona haja ya kuendelea na mfumo huo kwa kuwa ungesababisha migogoro isiyo ya lazima, ndiyo maana serikali kuanzia za vitongoji zinashughulia suala la ulinzi na usalama.

"Mabalozi wa nyumba kumi wanaweza kutoa taarifa za uhalifu kwa wajumbe wa serikali za mitaa ili nao wazifikishe mahali husika kwa ajili ya hatua zaidi zikiwamo za kisheria," anasema.

Anafafanua kuwa suala la ulinzi na usalama ni la kila Mtanzania katika eneo lake, na kwamba ndiyo maana katibu huyo anahimiza kamati hizo kuwatumia hata mabalozi wa nyumba kumi kwa ajili ya kupata taarifa sahihi.

"Moja ya maeneo ambayo Tanzania ilifanikiwa, katika utawala wa awamu ya kwanza wa Mwalimu Julius Nyerere ni katika ulinzi na usalama wa watu na mali zao kwa kutumia mabalozi hao," anasema.

### KULIKUWAPO MAFANIKIO

Wasira anataja hatua zilizochangia hilo, kuwa ni kuwapo kwa mabalozi hao, ambao walifanya kazi kwa umakini, na kwamba hakukuwa na mwanya wa mtu kwenda sehemu bila kujulikana.

"Kila mjumbe alifahamu idadi ya watu wake kuanzia majina, shughuli zao, na pia mgeni aligundulika kirahisi, kwani alipofika, mwenyeji wake, alilazimika kutoa taarifa kwa balozi wa nyumba kumi," anasema.

Wasira anataja miongoni mwa taarifa zilizokuwa zikichukuliwa kuwa ni jina la mhusika, ametoka wapi, amefika kufanya nini na atakaa kwa muda gani, pia wakati wa kuondoka, mwenyeji wake alimpeleka kwa balozi ili kuaga.

"Hata pale mtu alipokuwa akisafiri, jua likazama kabla ya hajafika kijiji anachokwenda, ilimlazimu aende kwa mjumbe kama hakuwa na ndugu, lengo likiwa ni kupata taarifa zake na pia kulinda usalama wake," anasema.

Anasema, mijini pia kulikuwa na utaratibu wake, kwa mtu kufika nyumba ya kulala wageni na kujaza taarifa zake kwa usahihi katika daftari, ambapo mfumo huo ulisaidia kudhibiti vitendo vya uhalifu wa aina mbalimbali.

# Wanawake wanavyokwazwa na uchaguzi majimboni Z'bar

## ▪ Fursa 50 wameambulia viti vinane

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

LICHA ya uchaguzi mkuu wa 2020 wanawake 61 kujitokeza kuchukua fomu kugombea nafasi ya uwakilishi kupitia vyama vingi vya siasa, idadi ya walioshinda majimboni na kuwa wabunge ni kiduchu.

Kinamama waligombea kwenye majimbo 50 ya Zanzibar lakini ni nane pekee walioshinda, wote kutoka CCM, wakati wanaume 190 waliojitosa 42, walishinda ndiyo maana watetezi wa haki za wanawake wanahoji inakuwaje? Katika mazingira hayo uwakilishi wa uwiano wa 50/50 unawezekana.?

Sababu zinazoelezwa kuwakwamisha mojawapo ni mfumo dume uliojengeka katika jamii kuwa kinamama hawafai kuwa viongozi.

Mwanaasha Khamis Juma ni miongoni mwa wanawake nane walioshinda uwakilishi katika majimbo kupitia CCM, akiliwakilisha jimbo la Dimani ambalo kwa mara ya kwanza nafasi ya uwakilishi inashikwa na mwanamke.

Anasema aliongoza kwa kura nyingi katika jimbo hilo na kuchaguliwa baada ya kuaminiwa na wananchi wa jimbo hilo na haikuwa jambo rahisi hadi kufanikiwa kupata nafasi hiyo, lakini alipitia changamoto nyingi za mifumo dume licha ya kuwang'oa wanasiasa nguli wanaume katika uchaguzi wa kura za maoni.

Mwanaasha ni miongoni mwa wanawake wachache waliomo ndani ya baraza la wawakilishi kutoka majimboni, kwenye uwakilishi huo wenye wanaume 42 kutoka majimbo 50 ya Zanzibar huku wanawake wakiwa wachache mno Mwanaasha amekuwa mwakilishi kwa awamu mbili , mwaka 2015 alikuwa mwakilishi wa Chukwani lakini baada ya jimbo hilo kugawanywa alijitosa kugombea uwakilishi Dimani, baada ya kutangazwa kuwa jimbo na kwamba alikuwa na washindani zaidi ya 10 kutoka CCM lakini alipambana kwa sera na hoja hadi kuibuka na ushindi na chama chake kumpitisha .

"Nilitembea usiku na mchana kuomba ridhaa ya kuchaguliwa kuwa mwakilishi na nawashukuru wananchi wa Dimani waliniamini na kunipa kura zao bila kujali mimi ni mwanamke,"anasema.

Anakumbusha kuwa maendeleo hayaletwi na wanaume pekee hata wanawake wana nafasi kubwa ya kuleta maendeleo hivyo amegombea jimbo hilo ili kushirikiana na serikali na wapigakura kuletea maendeleo wananchi.

Mwanaasha anasema kwa miaka mingi wanawake wamekua nyuma kugombea nafasi za uongozi hasa majimboni , jamii ikiwa na dhana kuwa mwanamke ni mama wa familia: "Tulikuwa nyuma katika nafasi za uongozi lakini sasa tumeamka na tunapambana na wanaume kushika nafasi za uongozi katika siasa."



Zena Ahmed Said, Katibu Mkuu Kiongozi wa SMZ, ni miongoni mwa wanawake wateule waandamizi. **PICHA MTANDAO.**

Mwanasiasa huyu ni mama wa familia, anasema mama wa familia siyo kikwazo kushindwa kuwahudumia wapigakura na katika kuwaletea maendeleo na kwamba baada ya kuingia barazani hakuridhika na nafasi hiyo pekee na aliamua kugombea nafasi ya Naibu Spika japo hakufanikiwa , lakini ni Makamu wa Baraza la Wawakilishi.

"Wanawake tunaweza mimi ni Makamu wa Baraza la Wawakilishi kwa kipindi cha pili, kuanzia mwaka 2015 niligombea na kushinda na mwaka huu nimeshinda tena, "anaongeza.

Baraza la Wawakilishi Zanzibar lina idadi ya wajumbe 75, wanaume ni 46 na wanawake ni 29 kati ya hao, majimboni kuna wanaume 42, wa kuteuliwa na Rais ni wawili wakati wanawake kutoka majimboni ni wanane, viti maalum ni 18 na walioteuliwa na Rais ni watatu.

Mtumwa Peya ni mwakilishi wa Bumbwini anayesema ushindi wake umetokana na nguvu kubwa ya wanawake wezake ambao ndiyo wapiga kura wengi na kuongeza:

> "Wanawake tunaweza mimi ni Makamu wa Baraza la Wawakilishi kwa kipindi cha pili, kuanzia mwaka 2015 niligombea na kushinda na mwaka huu nimeshinda tena, "anaongeza.

"Siyo wanawake pekee walionipigia kura hadi wanaume nao wamenipigia lakini niseme kuwa wanawake wakiwa wamoja wana nguvu kubwa ya kumsimamisha mwanamke kuwa kiongozi na akashinda kwa sababu idadi kubwa ya wanaopigakura ni kinamama."

Mtumwa analiongoza jimbo hilo tangu mwaka 2015 na sasa ni kipindi chake cha pili cha uongozi na aliwagaragaza wagombea wanaume wengi katika uchaguzi tangu mwaka 2015.

Anasema licha ya elimu ndogo aliyonayo lakini wapiga kura wake pamoja na chama chake hawakukiona kuwa ni kikwazo kufikia uongozi walimuunga mkono hadi kuibuka kidedea katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2020 kuweka historia kwa sababu ni kwa mara ya kwanza kuongozwa na mwanamke tangu uchaguzi wa vyama vingi mwaka 1995.

Asha Abdallah Mussa, ni mwakilishi wa Mahonda naye anashika nafasi hiyo kwa kipindi cha pili ambapo awali baada ya uchaguzi mkuu wa mwaka 2015 alikuwa akiwakilisha jimbo la Kitope lakini baada ya kugawa majimbo kulikofanywa na Tume ya Uchaguzi Zanzibar (ZEC) na kuondoshwa kwa jimbo hilo aliamua kugombea uwakilishi jimbo la Mahonda katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2015.

Asha kabla ya kuwa mwakilishi aligombea udiwani katika wadi ya Kilombero mwaka 2000 na kuibuka mshindi lakini hakuridhika na nafasi hiyo akapaa zaidi hadi kushinda uwakilishi.

### RAIS AWAFAGILIA

Rais wa Zanzibar Dk. Hussein Ali Mwinyi, anasema wanawake aliowateua na kuwapa nafasi mbalimbali za uongozi wanafanya kazi nzuri kuliko hata wanaume hivyo ataendelea kuwapa nafasi za uongozi.

Anasema anapofanya uteuzi wa viongozi hana ubaguzi wa kijinsia na huchagua kwa mujibu wa sifa na uwezo ikiwemo elimu bila ya kuzingatia jinsia.

"Niseme hadharani kuwa wanawake niliowapa nafasi za uongozi wanafanya kazi vizuri kuliko hata wanaume hivyo wanawake wana uwezo mkubwa,"anasema.

Anasema anaiongoza serikali bila ubaguzi wa kijinsia na kuwataka wanawake kuzidi kuchapa kazi ili kuendelea kuaminika katika jamii na kubadilisha mitazamo hasi dhidi yao.

Mkurugenzi wa Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake (TAMWA) Zanzibar Dk. Mzuri Issa, anasema mazingira ya kisiasa nchini yanatoa fursa kwa wanawake wengi kuwa viongozi serikalini na taasisi binafsi.

Anafafanua kuwa ni kufuatia Tanzania kuongozwa na Rais mwanamama Samia Suluhu Hassan.

Anaona kuwa mazingira yaliyopo hivi sasa ni wazi kuwa taifa limefunguka na fursa zaidi za wanawake wengi kuwa viongozi zinaonekana.

Anaeleza zaidi kuwa ushiriki wa wanawake katika nafasi hizo ni matakwa ya dunia yenye dhamira ya kuleta usawa kwa watu wote hivyo hakuna sababu mwanamke kuachwa nyuma.

### WANAUME WA MABADILIKO

Mwenyekiti wa Timu ya Wanaume wa Mabadiliko Zanzibar, Muhammed Jabir, anasema wamefanya kazi kubwa ya kutoa elimu kwa jamii kuhusu ushiriki wa wanawake katika nafasi za uongozi ambayo imefanikisha kupunguza mitazamo hasi kwa jamii kuhusu uongozi wa wanawake.

Anaeleza kuwa kabla ya uchaguzi mkuu wa mwaka 2020 waliwafikia wananchi katika maeneo mbalimbali vijijini kuwapatia elimu hiyo ambayo imefanikisha kupata wanawake nane walioshinda katika majimbo ya uchaguzi jambo ambalo tofauti na kwenye uchaguzi uliopita.

Anasema elimu zaidi inahitajika kwa jamii ili kufikia asilimia 50 kwa 50 katika vyombo vya maamuzi na kubadilisha mitazamo ya jamii kuwa mwanamke ni mwangalizi wa familia.

# Uhuru anapomkubali Raila uchaguzi 2022

## Ruto awekwa pagumu Gideon Moi amtosa

**Na Ani Jozeni**

RAILA Odinga, mgombea urais 2022 na kiongozi mkuu wa muungano wa CORD , ambaye amekuwa mshirika wa Rais Uhuru Kenyatta katika awamu yake ya pili, sasa ana uhakika zaidi wa kuchukua kijiti cha uongozi baada ya kukubaliwa rasmi na Kenyatta, anayemaliza muda wa uongozi.

Odinga aliyewahi kuwa Waziri Mkuu awamu ya tatu iliyoongozwa na Mwai Kibaki, amejihakikishia nafasi nzuri baada ya ujumbe mzito wa Mfuko wa Mlima Kenya ambao ni kundi la wanasiasa wa eneo la kati ya nchi hiyo ambako Rais Kenyatta ana ngome imara, kutoa rai ya kuwa pamoja naye katika mkutano mkubwa uliofanyika uwanja wa Kasarani jijini Nairobi wiki iliyopita.

Wanasiasa hao wanasema wanapendezwa na mipango ya Raila kuhusu eneo hilo, na hawataki mafisadi kukamata usukani.

Angalizo hilo ni kombora lililoelekezwa katika kambi ya Naibu Rais William Ruto, ambaye anamaliza muda wake katika nafasi hiyo ambako amekuwa na Rais Kenyatta tangu 2013, ila wakaanza mtifuano kuanzia 2018.

Ni wakati Rais Kenyatta alipoona ulazima wa kufikia muafaka wa kitaifa na upinzani, kuweka mpango wa pamoja wa utawala na hasa kupambana na rushwa iliyokithiri serikalini.

Ruto amekuwa akiongoza kambi ya wanaopinga maafikiano hayo, akitaka jadi iendelee, kuwa walioshinda watawale na walioshindwa wangoje wakati mwingine, ila siyo sasa.

**MOI AKIMBIA**

Baadhi ya wachunguzi wa habari nchini humo na mataifa jirani walishangazwa na uwepo wa mbunge mashuhuri Gideon Moi, mwanae hayati Daniel Arap Moi, aliyechukua nafasi ya urais baada ya kifo cha Rais Jomo Kenyatta mwaka 1978, na ambaye wakati wa utawala wake Raila Odinga aliwahi kuwa Katibu Mkuu wa chama tawala cha KANU.

Ndiyo chama ambacho hata leo mbunge Moi anakiongoza 'mabaki' yake na bila Ruto kuungwa mkono na Moi eneo la Rift Valley au Bonde la Ufa ambalo ni ngome yake, kura za eneo hilo zitatawanyika.

Kuwepo mawaziri kutoka ukanda mlima Kenya wakimuunga mkono Raila, pamoja na ujio wa Gideon Moi, vinampa Odinga tiketi ya kuingia kwenye uchaguzi mkuu kwa raha.

Mpangilio huo wa kujipanga kugombea urais katika uchaguzi mkuu unaotazamiwa kufanyika Agosti 2022 ni mwendelezo wa siasa za Kenya kuanzia kupatikana kwa uhuru Desemba 1963.



Rais Jomo Kenyatta, baba wa Uhuru. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

Misukosuko yake na jinsi dola ilivyojibadilisha katika mpangilio wa kuungwa mkono hadi sasa.

Wakati wa kufikia uhuru, viongozi wengine wa kisiasa akiwamo Daniel Arap Moi walikuwa tayari Kenya ipewe uhuru wake bila Mzee Jomo Kenyatta, kutolewa kizuizini Lodwar, alikozuiliwa huko kwenye eneo la kaskazini mashariki lenye ukame na jangwa.

Hata hivyo, Jaramogi Ajuma Ogiga Odinga, baba yake Raila Odinga, alikataa hakuwa tayari. Kenyatta akafunguliwa, akawa Waziri Mkuu na halafu Rais huku Odinga akiwa makamu wake hadi 1966 alipojiuzulu kwa ajili ya tofauti kali za sera na chuki za ukabila zilizopenya.

Hivyo, licha ya wachambuzi na wazungumzaji kisiasa kuchukulia siasa za Kenya kama zenye msingi wake katika ukabila, hali halisi ni kuwa sera ndiyo zinatawala, kuwa na uongozi wa juu nchini humo katika miongo takriban sita ya uhuru, umekuwa ukichelea na kuzuia kwa nguvu zote viashiria vya mapinduzi.

> Wakati wa kufikia uhuru, viongozi wengine wa kisiasa akiwamo Daniel Arap Moi walikuwa tayari Kenya ipewe uhuru wake bila Mzee Jomo Kenyatta, kutolewa kizuizini Lodwar, alikozuiliwa huko kwenye eneo la kaskazini mashariki lenye ukame na jangwa.



Jaramogi Oginga, baba wa Raila na mpinzani wa mzee Kenyatta.

Eneo la kati la Kenya lina mchanganyiko wa uhafidhina wa machifu waliowaunga mkono watawala wa Kiingereza wakati wa uasi ambayo wazawa wanayaita mapambano ya kuondoa walowezi wa Kizungu.

Wakuu wa maeneo mengine wamekuwa na viwango tofauti vya kusimamia uhafidhina japo lipo tatizo la utii kwa kiongozi mkuu halafu na hisia za mabadiliko.

Kukubaliwa rasmi kwa Raila Odinga na kambi ya wahafidhina kisera ya Rais Kenyatta na viongozi wengine wa ukanda wa Mlima Kenya ni kielelezo kuwa tishio hilo la cheche za mapinduzi halipo tena. Sasa ni wazi waziri mkuu huyo wa zamani anaaminika ni mshirika halisi wa kulinda kile kilichopo, na pia kuendeleza jitihada za serikali ya muhula wa pili wa awamu ya nne anayoiongoza Uhuru Kenyatta, za kukabiliana na ufisadi wa jadi serikalini, unaowasha mioto ya ukinzani miongoni mwa wananchi, na kuchochea ukabila. Ni ukabila wa kujikinga na lawama za ufisadi au wa kuungwa mkono kuleta mageuzi, ambao kimsingi ukabila wa Odinga ulikuwa huo wa kuleta mageuzi, na ukabila wa Ruto, kujihalalisha.

Ina maana kuwa sasa kuna uwezekano wa kijiti cha urais siyo kurudi kwa awamu ya pili ya rais nchini humo - iwe ni kikanda yaani kwa Wakalenjin kupitia Ruto kwani Gideon Moi bado anaelezwa kuwa ni mchanga kwa nafasi hiyo ila kurekebisha hitilafu za jadi na kijiti hicho kiende kwa mrithi wa Jaramogi.

Kama ambavyo Odinga baba alitetea maadili Kenya isipate uhuru bila Kenyatta kutolewa kizuizini, na akapinga sera za kukwapua mashamba kwa fedha za serikali ukifanywa na Rais Jomo Kenyatta na watu wake wa karibu, Odinga 'mtoto' amemsaidia Kenyatta 'mtoto' kukwepa dhoruba ya mgawanyiko na hata machafuko iliyokuwa ikiinyemelea Kenya. Ni pale Raila akiapishwa 'rais mbadala wa watu wa Kenya.'

Raila alitoa maagizo baada ya kuapishwa huko kuwa wafuasi wake wasinunue chochote katika biashara yenye uhusiano wowote na Rais Kenyatta, ambaye anajulikana zaidi kwa biashara ya maziwa ya kampuni ya Brookside, ila anazo biashara nyingine nyingi.

Waswahili wanasema 'akumulikaye mchana usiku hukuchoma,' hivyo kususia maduka na bidhaa hizo ingekuwa hatua ya kwanza, ya pili ni kutia kiberiti maduka, mashamba au viwanda vyenye alama hizo. Uhuru akaona yasifike huko, akamwita Raila wakaweka mpango wa kufumua mpangilio wa utawala na kurudisha imani ya wananchi.





## Tume yatia neno waliojifungua kurejea shuleni

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

TUME ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (THBUB) imeitaka serikali ikae na wadau mbalimbali wa elimu kuandaa na kupitia sera, sheria na miongozo itakayosimamia utekelezaji wa wanafunzi waliopata ujauzito wakiwa shuleni, kuendelea na masomo.

Vilevile, tume hiyo imeitaka serikali iweke mazingira wezeshi kwa watoto wanaorejea shuleni kuendelea na masomo baada ya kujifungua bila kuwapo na unyanyapaa na ubaguzi kutoka kwa wanafunzi wenzao na walimu.

Kamishna wa Tume hiyo, Dk. Fatma Khalfan, alitoa rai hiyo wakati wa maadhimisho ya Siku ya Haki za Binadamu Duniani yaliyofanyika jijini hapa jana.

Dk. Fatma alitoa pongezi kwa serikali kutokana na uamuzi wa kuwarejesha shuleni wanafunzi waliokatisha masomo yao kutokana na kupata ujauzito.

"Tukielekea katika kilele cha maadhimisho ya Siku ya Haki za Binadamu Duniani, Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora tunatoa pongezi kwa serikali kwa uamuzi wake wa kuwarejesha shuleni wanafunzi waliopata ujauzito," alisema Dk. Fatma.

Alisema THBUB imefurahishwa na uamuzi huo na inapenda kutoa pongezi zake za dhati kwa serikali kwa hatua yake hiyo inayowahakikishia watoto nchini haki yao ya msingi ya kupata elimu bila ya ubaguzi wa aina yoyote.

Vilevile Dk. Fatma alisema uamuzi huo wa serikali ni utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu ya Umoja wa Mataifa (SDG) yanayolenga kuhakikisha hakuna anayeachwa nyuma katika maendeleo na kuhakikisha elimu jumuishi na bora kwa wote.

Hata hivyo, Dk. Fatma aliwataka wazazi, viongozi na jamii kwa ujumla, waongeze nguvu katika kutoa na kusimamia malezi bora ili kutokomeza mimba katika umri mdogo.

Ofisa Habari wa Umoja wa Mataifa (UN) Tanzania, Stella Vuzo, alisema wameadhimisha Siku ya Haki za Binadamu kwa kufanya mdahalo wa wazi kwa wanafunzi wa sekta ya sheria wa Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM) na wameangazia kaulimbiu ya mwaka huu kupunguza tofauti ili kuleta haki za binadamu.

Vuzo aliwataka wanafunzi hao kujua katika jamii kuna suala la haki za binadamu na kusiwapo tofauti ili watu wasichelewe kupata haki.

# Udumavu tatizo nchini

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

SERIKALI imezindua Programu Jumuishi ya Taifa ya Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto huku Tanzania ikitajwa kuwa moja kati ya nchi za Afrika zenye idadi kubwa ya watoto wenye utapiamlo.

Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Dorothy Gwajima, alibainisha hayo juzi jijini Dodoma katika hotuba yake kwenye hafla ya uzinduzi wa programu hiyo.

Alisema utafiti wa hali ya lishe uliofanywa na Taasisi ya Chakula na Lishe (TFNC) kwa kushirikiana na Ofisi ya Taifa ya Takwimu mwaka 2018, ulibainika kuwa zaidi ya watoto milioni 2.6 wenye umri chini ya miaka mitano nchini wamedumaa.

"Idadi kubwa ya watoto hao iko katika mikoa 11 ambayo ni Dar es Salaam, Kagera, Kigoma, Mara, Dodoma, Geita, Tanga, Ruvuma, Mbeya, Morogoro na Tabora," alisema.

Waziri huyo alisema zaidi ya watoto 270 walio chini ya umri wa miaka mitano nchini hupoteza maisha kutokana na matatizo yanayohusiana na lishe duni.

"Asilimia 40 ya vifo hivyo hutokea katika mwezi wa kwanza wa maisha ya watoto hao. Tukumbuke kuwa baadhi ya mikoa inayoongoza kwa tatizo la lishe ina kiwango cha juu cha upatikanaji wa chakula nchini," alifafanua.

Alisema programu hiyo inalenga kuchangia katika kumaliza vikwazo vya lishe kwa watoto chini ya miaka minane.

"Malezi yenye mwitikio ni huduma muhimu sana kwa mtoto mwenye umri mdogo ambapo mzazi au mlezi anahitajika kuwa karibu na mtoto na kumhusisha katika shughuli mbalimbali zinazoweza kuchangia uchangamshi wake.

"Pia huduma hizi humwezesha mzazi kutambua matatizo ya kiafya, lishe na usalama wa mtoto ili kubaini mapema changamoto na kuchukua hatua stahiki," alisema Dk. Dorothy.

Alisema huduma hizo hazipatikani kwa utimilifu katika jamii kwa sababu ya kukosa uelewa na nafasi finyu ya wazazi au walezi ya kuwa karibu na watoto wao.

Waziri huyo alisema hali hiyo inapelekea watoto wengi kutokuwa na uangalizi wa karibu, hivyo mtoto kuwa hatarini kufanyiwa ukatili na hata kupata magonjwa ambayo ni kikwazo cha ukuaji wake.

Alisema wazazi au walezi kukosa mbinu za kufuatilia mienendo na usalama wa watoto ni tatizo kubwa katika malezi ya watoto nchini.

"Ndugu washiriki, suala la ujifunzaji wa mtoto linaanza punde tu mtoto anapozaliwa, ujifunzaji unaendelea kadri mtoto anapoendelea na ukuaji wake," alisema.

Aliongeza kuwa ujifunzaji wa awali wa mtoto una mchango mkubwa kwa ukuaji wa ubongo wa mtoto kwa takribani asilimia 80 ambao unamwandaa mtoto kuwa mwenye uelewa na uwezo mkubwa wa kupambanua mambo katika kipindi cha ukuaji wake hadi anapokuwa mtu mzima.

Hata hivyo, alisema kuna watoto wachache wanaopata fursa ya ujifunzaji wa awali wakiwa katika umri chini ya miaka tano.

"Taarifa ya mikoa kuhusu vituo vya uchangamfu wa awali wa watoto kutoka Ofisi ya Rais TAMISEMI ya mwaka 2018 inonyesha kuwa kulikuwa na vituo 5,274 vya kulea watoto mchana kwenye mikoa 16 ya Tanzania Bara na jumla ya watoto 1,003,291 walikuwapo katika vituo hivyo na kati ya vituo hivyo, 135 ni vya binafsi na 78 vinamilikiwa na mashirika ya dini na 48 vya serikali," alisema.

Akizungumzia ukatili dhidi ya mtoto, waziri huyo alisema bado ni kero kubwa nchini.

"Kwa mujibu wa taarifa ya Ukatili wa Kijinsia wa Jeshi la Polisi nchini, katika mwaka mmoja uliopita, matukio yameongezeka kutoka 15,680 kwa mwaka 2019 hadi matukio 15,870 kwa mwaka 2020," alisema.

Mwakilishi Mkazi wa Shirika la Kimataifa la Watoto (UNICEF), Shalin Bahuguna, alisema watashirikiana na Serikali ya Tanzania katika kuhakikisha programu hiyo inafanikiwa ili kuwa na taifa bora.



Ofisa wa Ofisi ya Rais, Maadili ya Uongozi wa Umma, Evarist Msakila (watatu kushoto), akimkabidhi cheti mmoja wa wahitimu wa darasa la awali ya shule ya Ilakozi wakati wa mahafali ya shule hiyo, Nzunguni, jijini Dodoma mwishoni mwa wiki. Wapili kulia ni Mkurugenzi wa shule hiyo, Olipa Mkuyu. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Mfumo Montessori wapigiwa chapuo

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

MWENYEKITI wa Montessori Community of Tanzania (MCT), ameishauri jamii kutumia mfumo wa ufundishaji wa Montessori kwa kuwa unamsaidia mtoto kukua katika maisha na si kielimu peke yake.

Martha Dello alitoa rai hiyo jana alipozungumza na waandishi wa habari katika banda lao la maonyesho kwenye uzinduzi wa programu jumuishi ya taifa ya malezi, makuzi na maendeleo ya awali ya mtoto uliofanyika jijini Dodoma.

Dello alisema mfumo huo una maeneo matano yanayosaidia kumkuza mtoto na kumwendeleza katika nyanja zote kwa vifaa na vitendo vya kawaida.

"Maria Montessori alisema ya kwamba hatuwezi kuwakinga watoto wetu na maisha, tunaweza kuwaandaa watoto wetu na maisha, kwenye darasa la Montessori tunatumia vifaa zaidi kama mnavyoona hapa, tuna maeneo matano yanayomkuza na kumwendeleza mtoto kuna vitendo vya kawaida.

"Tunaposema vitendo vya kawaida ni vile vinavyofanyika kwenye maisha yetu ya kila siku kwa kufagia, kuosha vyombo, vinamsaidia kujitegemea, kuwajibika kwenye maisha yake.

"Vitendo hivi baadaye vinamsaidia kwenye kuandika, anakuza misuli yake, kuna vitendo vya milango ya fahamu," alisema.

Alibainisha kuwa vitendo hivyo vya milango ya fahamu husaidia kubaini kama kuna mtoto ana tatizo na kupelekwa hospitalini.

"Tunamfundisha mtoto lugha ambayo ni muhimu katika mawasiliano, mambo ni mengi katika Montessori, kuna vyuo vinatoa mafunzo kwa mfumo huu, kuna madarasa ya awali yapo mikoa yote Tanzania yanafundisha kwa mfumo huu," alisema.

Mkurugenzi wa MCT, Sarah Kiteleja, alisema mfumo huo unamsaidia mtoto kujitambua, kupata ujuzi na ujasiri wa kufanya vizuri kwenye maisha yake.

"Tunafanya kazi na jamii, tunahamasisha serikali ichukue mbinu hii ya ufundishaji ili kusaidia watoto wa Kitanzania kuwa na weledi wa kufanya vizuri na kuwa na ubunifu," alisema.

Aliongeza kuwa watoto wengi wa Kitanzania wananyanyasika kutokana na malezi mabaya na kwamba mfumo huo unamponya mtoto na kuwa na utu.





# Wanakijiji wapata ukombozi wa zahanati

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WAKAZI wa Kijiji cha Shitete kilichoko Kata ya Isuto katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, wameondokana na adha ya kutembea umbali wa zaidi ya kilomita 20 kwenda kupata matibabu katika Mji wa Mbalizi, baada ya kujengewa zahanati.

Zahanati hiyo imejengwa kwa ushirikiano kati ya Serikali na Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (UNICEF), ambapo wananchi hao wanadai kuwa walikuwa wanalazimika kuwabeba wagonjwa kwenye machela.

Zahanati hiyo pamoja na miundombinu mingine, imejengwa na UNICEF kupitia mradi wake wa SAWA, ambapo ulikabidhiwa juzi serikalini na kushuhudiwa na wananchi wa kijiji hicho cha Shitete ambao ndio wanufaika na mradi.

Wakizungumza wakati wa makabidhiano ya mradi huo, wakazi wa kijiji hicho walisema utawasaidia kupata huduma za afya karibu na makazi yao tofauti na ilivyokuwa awali ambapo walikuwa wanalazimika kutembea umbali mrefu.

Mmoja wa wananchi hao, Vicky Kinyongo, alisema wanakijiji walikuwa wanalazimika kuwabeba wagonjwa kwa machele kutokana na miundombinu ya barabara za eneo hilo kutoruhusu usafiri wa vyombo vya moto.

Alisema wajawazito walikuwa wanasafirishwa umbali mrefu hali ambayo ilikuwa inahatarisha maisha yao na vichanga vyao huku akidai kuwa daraja walilokuwa wanalitumia kuvuka na pikipiki lilivunjika.

"Tunashukuru serikali mradi huu utatusaidia sana, sasa tumeondokana na adha ya kubebana mzega mzega kwenye machela kwenda hospitalini, wajawazito ndio tulikuwa tunapata shida sana, sasa hivi wametuwekea mazingira ya kujifungulia hapahapa," alisema Vicky.

Naye Simba Mwasenga, alisema wananchi walikuwa hawana uwezo wa kukamilisha ujenzi wa zahanati hiyo na kwamba serikali na UNICEF wasingeweza kukamilisha mradi huo.

Alisema wananchi wa eneo hilo wamepata shida kwa muda mrefu bila kupata ufumbuzi jambo ambalo alidai lilikuwa linawatia hofu mwaka huu endapo mvua ingeanza kunyesha bila zahanati hiyo kukamilika.

Akizungumza wakati wa kukabidhi mradi huo, Mwakilishi wa Mradi wa SAWA, Joachim Asenga, alisema pamoja na kukamilisha ujenzi wa mradi huo pia wameweka miundombinu mingine muhimu ambayo itawasaidia wananchi hao kupata huduma bila shida.

Alisema wamejenga vyoo matundu matatu kwa ajili ya wagonjwa, matundu matatu kwa ajili ya watumishi na tundu moja kwa ajili ya wajawazito wanaokwenda kujifungua kwenye zahanati hiyo.

"Pia tumeweka mfumo wa maji ambapo tumechimba kisima kimoja kirefu ambacho kina maji yenye uwezo wa kutosheleza mahitaji ya kijiji kizima, hivyo leo tunawakabidhi miundombinu hii ili mwendelee kuitunza na kuitumia," alisema Asenga.

Akipokea mradi huo kwa niaba ya serikali, Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, Ezekia Soda, alisema zahanati hiyo itawasaidia wananchi zaidi ya 7,000 wakiwamo wa vijiji jirani.

Aliishukuru UNICEF kwa kusaidia mradi huo, na kwamba serikali itaendelea kushirikiana na shirika hilo ili kutekeleza miradi mingine muhimu.



Mjumbe wa Serikali ya Kijiji cha Shitete, Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, Simba Mwasenga (kulia), akimkabidhi zawadi ya mbuzi dereva wa Shirika la SAWA, Alfred Myemba kama shukurani kwa Shirika la Umoja wa Mataifa la kuhudumia Watoto (UNICEF) kwa kuwajengea zahanati katika kijiji hicho juzi. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# TEMESA yaja na ufumbuzi tatizo la ajira

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WAKALA wa Ufundi na Umeme (TEMESA), umeamua kusaidia kupunguza tatizo la ajira nchini kwa kutoa fursa kwa vijana kwenda kupata mafunzo ya ufundi kwenye taasisi hiyo ili wapate ujuzi utakaowawezesha kujiajiri.

Akifungua bonanza la michezo la wafanyakazi wa TEMESA kutoka mikoa sita ambalo lilifanyika juzi mkoani Mbeya, Mwakilishi wa Mkurugenzi Mkuu wa TEMESA, Mhandisi, Adelard Kweka, alisema taasisi hiyo imeamua kuwasaidia vijana kupata ujuzi wa aina mbalimbali ili waweze kuutumia ujuzi huo kuisaidia jamii na kujiajiri wenyewe.

"Kwa sasa TEMESA kupitia ofisi zetu zilizopo kila mkoa zinawakaribisha vijana kuja kujifunza ujuzi wa aina mbalimbali ili ujuzi uwasaidie kujiajiri na wengine kwa kutumia ujuzi huo wanaweza kuajiriwa kirahisi," alisema Kweka.

Alisema vijana watakaokwenda kujifunza TEMESA watapata ujuzi wa aina mbalimbali kama vile kutengeneza magari, umeme, kukarabati vivuko, mitambo, viyoyozi vya magari.

Alisema mbali na kutoa fursa hiyo kwa vijana, TEMESA pia inalo jukumu la kutengeneza magari yote ya serikali, kusuka mifumo ya umeme kwenye majengo ya serikali, kutengeneza na kukarabati vivuko na mitambo ya umma.

Meneja wa TEMESA mkoa wa Mbeya, Mhandisi Said Mawazo, alisema taasisi hiyo pia inatoa huduma zake kwa watu binafsi pale wanapokuwa na uhitaji.

Aliwataka wananchi kuchangamkia huduma zinazotekelezwa na wakala huo hasa vijana ambao wanafanya kazi kwenye karakana za watu binafsi ili wapate mafunzo sahihi ambayo yatawasaidia kwenye maisha yao.

Alisema serikali ilianzisha wakala huo kwa ajili ya kuwa na chombo maalumu ambacho kinatekeleza miradi ya umma ikiwamo matengenezo ya vivuko na mitambo mingine ya serikali.

Aliwataka wananchi wa Mkoa wa Mbeya kutumia mafundi wa taasisi hiyo kufanya uchunguzi wa mifumo ya vyombo vyao ili kuhakikisha wanatumia vyombo imara.

"Sisi tuna kila kitu lakini kuna uwezekano wananchi wengi hawajui shughuli zetu, ndio maana sasa hivi tumeamua kuja kuzitambulisha kwao ili wazijuwe na wazitumie," alisema Mawazo.

Alisema wakati wa bonanza hilo walikuwa wanatoa huduma hizo bure kwa wananchi na kwamba walikuwa wamebeba vifaa vyote kwa ajili ya shughuli hiyo.

Nao baadhi ya wananchi waliohudhuria bonanza hilo walisema walikuwa hawatumii huduma za wakala huo kutokana na kutokuwa na elimu ya kutosha kuhusu taasisi hiyo na huduma zake.

Mmoja wa wananchi hao, John Mwasumbi alisema alikuwa anaamini kuwa TEMESA wanashughulikia vyombo vya serikali pekee na hakuwahi kujua kwamba hata vyombo vya watu binafsi.

Aliwataka vijana kuchangamkia fursa zilizotangazwa na wakala huo ili na wao wanufaike na wawe na uwezo wa kuajirika na kujiajiri ili kuondokana na tatizo la ajira.

# Wataka kuboreshwa barabara za mitaani

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WAKAZI wa Mtaa wa Gombe Kusini Kata ya Itezi katika Halmashauri ya Jiji la Mbeya, wameomba serikali kuwaboreshea barabara za mitaa wakidai mvua ikinyesha maji yanakosa uelekeo na kujaa kwenye nyumba zao.

Wakizungumza na Nipashe jana, wananchi hao walisema barabara za mitaani zipo lakini hazijawekewa miundombinu mizuri ya maji hali ambayo inasababisha mafuriko kwenye maeneo ya makazi yao.

Hamis Mwasenga aliiomba serikali kuwaboreshea miundombinu hiyo kabla mvua haijaanza kunyesha nyingi, akidai kuwa kutokana na makazi holela maji hayana uelekeo.

Alisema serikali wakati mwingine huwa wanalazimika kuwapeleka watoto wao shuleni na kwenda kuwachukua wakati wa kurudi kutokana na kuhofia kusombwa na mafuriko.

"Kama unavyoona hapa maji huwa yanajaa hapa na hayana kwa kwenda, hizi nyumba maji huwa zinaingia miaka yote kutokana na maji yanayotoka kule juu yanakuja kupita hapahapa," alisema Mwasenga.

Naye Neema Mwaijande, alisema barabara ya lami imepita upande wa Gombe Kasikazini, lakini mifereji mingi imeelekezwa upande wao, hali ambayo pia imechochea mafuriko kwenye maeneo yao.



# Fomu maadili zawatia mtegoni 'vigogo' 50

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, ameutaka uongozi wa Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma kujiridhisha sababu za viongozi 52 kushindwa kurejesha fomu za tamko la rasilimali na madeni kwa wakati uliowekwa na kuwachukulia hatua stahiki za kisheria.

Dk. Mwinyi aliyasema hayo juzi katika kilele cha maadhimisho ya Siku ya Maadili na Haki za Binadamu, hafla iliyofanyika kwenye Ukumbi wa Sheikh Idrissa Abdul-Wakili, Kikwajuni Zanzibar.

Alisema katika mwaka wa fedha wa 2020/21, jumla ya viongozi 2,578 walichukua fomu za tamko la rasilimali na madeni ambapo viongozi 2,526 walirejesha fomu hizo kwa wakati mwafaka na viongozi 52 walirejesha fomu hizo nje ya muda uliowekwa.

Alisema viongozi waliorejesha fomu hizo nje ya wakati uliowekwa ni namna ya viongozi wanaopewa kazi na kuacha kuzifanya na pale inapotokea wakafanya, hukamilisha kwa wakati wanaopenda wao. Dk. Mwinyi aliwakumbusha viongozi wote wa umma waliotajwa katika Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma kuhakikisha wanarejesha fomu hizo baada ya kuzijaza sio zaidi ya Desemba 31, mwaka huu.

Akizungumzia tatizo la baadhi ya viongozi katika kujaza fomu hizo eneo linalohusu mapato ya biashara, Dk. Mwinyi alisema fomu mpya iliyofanyiwa marekebisho ambayo itatumika mwaka huu imezingatia suala hilo, hivyo akawataka viongozi kuijaza vizuri ikiwa na taarifa zote muhimu zinazohitajika.

Aliutaka uongozi wa tume hiyo kuendelea kushughulikia malalamiko yanayowasilishwa na wananchi kuhusu matumizi mabaya ya madaraka, udhalilishaji, mgongano wa kimaslahi na tuhuma za rushwa na wizi pamoja na vitendo visivyoridhisha katika jamii.

Rais Dk. Mwinyi alisema taarifa zinabainisha katika kipindi cha kuanzia Januari hadi Novemba mwaka huu, kumekuwa na tuhuma 289 zinazohusiana na vitendo vya rushwa na uhujumu uchumi ambazo zimechunguzwa.

"Hata hivyo, ninawataka Mamlaka ya Kuzuia Rushwa (ZAECA) kuongeza kasi ya uchunguzi kwani taarifa zinaeleza ni majalada 29 pekee ndio yaliowasilishwa Ofisi ya DPP," aliagiza. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais (Katiba), Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Haroun Ali Suleiman, aliwataka wateule wote wa Rais kufuata mwenendo wa kiutendaji wa kiongozi huyo na kumsaidia kikamilifu ili kufanikisha azma ya kujenga Zanzibar kwa kuzingatia uzalendo, uwajibikaji na uadilifu.

Mwenyekiti wa Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma, Asaa Ahmada Rashid, alisema katika kuimarisha taasisi zilizomo kwenye tume hiyo, Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora inaendelea kuzifanyia marekebisho sheria mbalimbali zinazoongoza taasisi hiyo ili kutekeleza vyema majukumu yake.

## Yatakayojiri mkutano Baraza la Wawikilishi sasa yawekwa bayana

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

MKUTANO wa tano wa Baraza la 10 la Wawakilishi Zanzibar unatarajiwa kuanza leo, maswali 152 yakitarajiwa kujibiwa katika mkutano huo.

Akizungumza jana na waandishi wa habari ofisini kwake Chukwani, Katibu wa Baraza hilo, Raya Issa Mselem, alisema miswada miwili itawasilishwa kwa hati za dharura katika mkutano huo.

Alitaja miswada hiyo kuwa ni Muswaada wa Sheria wa Kuanzisha Mamlaka ya Udhibiti wa Dawa za Kulevya wa Mwaka 2021 na Muswada wa Sheria wa Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2021.

Alibainisha kuwa katika mkutano huo pia kutakuwa na taarifa ya serikali kuhusu ripoti tano za utekelezaji wa kazi za Tume ya Maadili kwa Mwaka 2020/21.

Taarifa zingine ni pamoja na taarifa ya serikali kuhusu hali ya mazingira na hoja ya Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi kuhusu jumuiya ya wawakilishi kuhusiana na mabadiliko ya tabianchi Zanzibar.

"Pia kutakuwa na uwasilishaji wa hoja ya mjumbe kuhusu kuanzishwa kwa mtandao wa wabunge wa Afrika wa kupambana na rushwa Kanda ya Zanzibar," alisema.

Katibu huyo pia alisema kutakuwa na hoja itakayowasilishwa na mjumbe wa baraza hilo kuhusu kuanzishwa kwa Jumuiya ya Wawakilishi kuhusu idadi ya watu na maendeleo ya Zanzibar.



Meneja Uhusiano kwa Jamii wa Mgodi wa Barrick North Mara, Gilbert Mworia (kushoto), akifafanua jambo kwa wanufaika wa Programu ya Maendeleo ya Biashara za Ndani, walipotembelea mgodi huo, mkoani Mara hivi karibuni. Programu hiyo inatekelezwa na kampuni ya Kengo Ltd ili kuziwezesha kampuni za ndani kunufaika na fursa zilizoko kwenye sekta ya madini. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Makamu Rais apongeza utendaji Taasisi Uongozi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MAKAMU wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla, ameipongeza Taasisi ya Uongozi kwa kuendelea kujitolea katika kuwapatia mafunzo viongozi na watendaji wa serikali kupitia semina wanazoziandaa.

Hemed alitoa pongezi hizo alipofungua mafunzo ya uandaaji wa sera yaliyowashirikisha mawaziri, makatibu wakuu na manaibu katibu wakuu yaliofanyika katika ukumbi wa Golden Tulip Uwanja wa Ndege Zanzibar jana.

Alisema Taasisi ya Uongozi imekuwa mstari wa mbele katika kuisaidia Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kupitia semina elekezi wanazozitoa kwa viongozi na watendaji wa serikali.

Makamu wa Rais alisema nchi haiwezi kuwa na sheria ambayo haielekezi katika kuwaletea wananchi wake maendeleo kupitia sera zinazotengenezwa na taasisi husika.

Hemed aliwataka washiriki wa mafunzo hayo kushiriki kikamilifu kwa lengo la kujenga uelewa wa pamoja utakaowasaidia kutengeneza sera bora baada ya mafunzo hayo.

"Niwaombe tushiriki kikamilifu ili kujenga uwelewa wa pamoja," alisema.

Katibu Mkuu wa Baraza la Mapinduzi na Katibu Mkuu Kiongozi, Zena Ahmed Said, alisema mafunzo hayo yameandaliwa kwa lengo la kujenga uelewa kwa watendaji juu ya uandaaji wa sera mbalimbali katika taasisi za serikali.

Alisema kuwa kupitia mafunzo hayo, washiriki wataanza na utengenezaji wa sera ya uchumi wa bluu kwa vitendo, sekta ambayo serikali imeweka kipaumbele katika kukuza uchumi wake.

Katibu Mkuu Wizara ya Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais - Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi, Thabit Idarous Faina, alisema kwa sasa serikali imeandaa utaratibu maalumu wa ufuatiliaji wa uandaaji wa sera ili kupata sheria nzuri zitakazokuwa na mpango kazi kwa ajili ya kurahisisha utekelezaji wake.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## NYUMBA INAUZWA.

NYUMBA YA GOROFA INAUZWA IPO UKONGA,INAFREM NANE ZOTE ZINA WAPANGAJI,INAFAA KWA MAKAZI AU BIASHARA,BEI MAELEWANO(WAWEZA LIPA KWA **AWAMU) SIMU.0715 244754**

## NYUMBA INAUZWA.

NYUMBA INAUZWA MOROGORO MJINI MASIKA MIL. 100. NI NZURI KWA BIASHARA, INA VYUMBA KUMI NA NNE. KWA MAWASILIANO PIGA SIMU NAMBA: **0745 222 312 / 0715 768 8**

OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.
MOB: +255 - 0782253676

## UPOTEVU WA KADI ZA MAGARI

**GUO QIBING CHINESE**
ENGINIARING
MTAJWA HAPO JUU ANATANGAZA KUPOTELEWA KADI ZA MAGARI: ZENYE NAMBA ZA USAJILI, No.T 387 AVR-AINA YA BENZI CHASSIS No.62413215230498 NA KADI YA GARI AINA YA MD 50974-MANI YENYE NAMBA ZA USAJILI REG No.T 458 AAG PAMOJA NA KADI YA GARI AINA YA MISTUBISH REG No.T 672 AGY, CHASSIS No.FV415 J-443308.
TAARIFA YA POLISI NI KUMB No.MBE/MBE/RB/577530/2021

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**(MCA/63)**
**Katika Mahakama ya Mwanzo Muleba –Mjini**
**Wilaya ya Muleba**
**TALAKA MADAI NO 15/ 2021**
**Kwa GIDION JOHN WA KEMONDO**

Unaamrishwa na **JAMHURI** uhudhurie mbele ya Mahakama hii siku ya Alhamisi tarehe **16/12/2021 saa 2:00** asubuhi kuwa na mdaiwa katika shauri lililoko mbele ya mahakama hii ukifika usiondoke bila ya ruhusa ya mahakama na unaonywa kwamba usipuuzie wito huu.

Ukipuuzia wito huu bila udhuru kwa maana hati itaelewa kukulazimisha kuhudhuria .

Hati hii imetolewa kwa amri yangu na mhuri wa mahakama hii leo **tarehe 6/12/2021** kuitwa shaurini kwa maombi ya **MAKILINA JUSTINIAN**

6/12/2021

## WANTED



**IDDI RAMADHANI MWINYIGOHA** whose picture is provided above, is wanted by police of Tanzania. He is accused of criminal offense. To anyone who will see him please report to the nearest police station.
**RB No. STK/RB/7801/2021.**

## PASSPORT IMEPOTEA



**BETNESS SYLIVESTER TIBAIJUKA** anatangaza kupotelewa na **PASSPORT No. TAE135388** Iliyotelewa mwaka 2019 na kuisha 2029. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
Taarifa polisi:
**DOD/DOD/RB/587238/2021**

## KUPOTEA KWA VYETI



**BETNES ASIIMWE SYLVESTER** natangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne **index No. S0482-0008** Shule ya Sekondari ILUHYA mwaka 2009, Kidato cha Sita index No **S4419-0510** Shule ya Sekondari LUKOLE mwaka 2012 na cheti cha chuo **No.41683 SAINT AUGUSTINE UNIVERSITY OF TANZANIA** mwaka 2015. Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
Taarifa polisi: **DOD/DOD/RB/512276/2021.**

KIBAIGWA AUCTION MART & CO. LTD COURT BROKER

## TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

TUTAFANYA MNADA TAREHE **13/01/2022** SAA NNE ASUBUHI WA KUUZA GARI AINA YA **MARK X T 481 CXX,** MALI YA **ALLY S. MLUPILO** BAADA YA KUSHINDWA KULIPA MKOPO ALIYOKOPA IMARISHA MAISHA LIMITED, **P.O. BOX4169 DODOMA.** MNADA UTAFANYIKA NYERERE SQUARE, HIVYO TUNAPENDA KUWATANGAZIA WAHITAJI WOTE.

**KWA MAWASILIANAO PIGA NO. 0688729841/0784718272.**

KIBAIGWA AUCTION MART & CO. LTD COURT BROKER

## TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

TUTAFANYA MNADA TAREHE **13/01/2022** SAA NNE ASUBUHI WA KUUZA GARI AINA YA **TOYOTA SPACIO T 900 CTC,** MALI YA SILAS SYLIVESTER MAKANYANGA BAADA YA KUSHINDWA KULIPA MKOPO ALIYOKOPA IMARISHA MAISHA LIMITED, **P.O. BOX4169 DODOMA.** MNADA UTAFANYIKA NYERERE SQUARE, HIVYO TUNAPENDA KUWATANGAZIA WAHITAJI WOTE.

**KWA MAWASILIANAO PIGA NO. 0688729841/0784718272.**

KIBAIGWA AUCTION MART & CO. LTD COURT BROKER

## TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

TUTAFANYA MNADA TAREHE **13/01/2022** SAA NNE ASUBUHI WA KUUZA GARI AINA YA **TOYOTA SPACIO T 900 CTC,** MALI YA SILAS SYLIVESTER MAKANYANGA BAADA YA KUSHINDWA KULIPA MKOPO ALIYOKOPA IMARISHA MAISHA LIMITED, **P.O. BOX4169 DODOMA.** MNADA UTAFANYIKA NYERERE SQUARE, HIVYO TUNAPENDA KUWATANGAZIA WAHITAJI WOTE.

**KWA MAWASILIANAO PIGA NO. 0688729841/0784718272.**

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**

**Probate and Administration Cause No……… of 2021**

**In the matter of the estate of the late SAMAMBA CHELEA MDONONDO of Kisasa within Dodoma City**

**And**

**In the matter of application for letters of administration by JENIVA CHIMBWI MHAKA**

**PETITION FOR LETTER OF ADMINISTRATION WHEN THE DECEASED DIED INTESTATE**
**(SECTION 56)**

**GENERAL CITATION**

**(Rule 75 probate Rules GN no.369 of 1963)**

ALL PERSONS claiming to have any interest in the estate of the above named deceased person are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 16th day of December, 2021.
Dated at Dodoma this 22ND day of November,2021.

RESIDENT MAGISTRATE

DRAWN AND FILED BY:

*Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676*

Kwa Habari Motomoto
usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku
Tupigie 0782253676
Nipashe MWANGA WA JAMII

OFISI ZA MATANGAZO
MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,
PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.
E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## HABARI KIMATAIFA

# Gbagbo ataka waliokimbia nchi warejee

**Accra,** GHANA

RAIS wa zamani wa Ivory Coast, Laurent Gbagbo (pichani chini), amesema raia wa nchi hiyo 11,000, waliokimbilia baada ya kuzuka machafuko yaliyosababishwa na uchaguzi, warejeshwe nchini humo.

Gbagbo, kwa muda wa siku nne alifika Ghana kushiriki mazishi ya Kapteni Kojo Tsikata, ambaye alikuwa ofisa mwenye ushawishi na mshirika wa karibu wa rais wa zamani wa Ghana, Jerry Rawlings.

Akiwa nchini Ghana, Gbagbo, pia aliwatembelea wakimbizi ambao anataka warejee Ivory Coast.

Damana Adia Pickass pamoja na Justin Koné Katinan, kiongozi wa zamani wa Chama cha Ivorian Popular Front ni miongoni mwa watu maarufu zaidi na wanaomuunga mkono Gbagbo, waliolazimika kutoroka Ivory Coast na kukimbilia Ghana, na walirejea Ivory Coast msimu wa masika uliopita.

Wafuasi wa Laurent Gbagbo ni takribani 7,400, wako uhamishoni nchini Ghana, kulingana na Chama cha PPA-CI, chama kipya cha rais huyo wa zamani.

Rais huyo wa zamani, alikutana na wawakilishi wa wakimbizi hao mwishoni mwa wiki, mjini Accra.

"Mkutano usio rasmi ambao haukupangwa katika programu," alisema Ousmane Sy Savané, Meneja wa Mawasiliano wa Chama cha PPA-CI. Mkutano, hata hivyo, ni muhimu, lakini suala hili bado ni gumu."

Mwaka 2015, Shirika la Umoja wa Mataifa linalohudumia Wakimbizi (UNHCR), lilisitisha kutoa huduma ya kifedha kwa raia hawa wa Ivory Coast, waliokuwa uhamishoni, maofisa wa zamani na wadau katika masuala ya kiuchumi.

Walikataa mara kwa mara, wakidai kuachiliwa kwa Laurent Gbagbo, kama sharti.

Baada ya zaidi ya miaka 10, uhamishoni, kurejeshwa nyumbani kwa wakimbizi hao, kunamaanisha gharama kubwa kwa familia hizi, ambazo zinabaini kwamba faranga za CFA 300,000 zinazotolewa na UNHCR hazitoshi kama fidia kwao.

Vyama vya upinzani vinatarajiwa kuanza tena rasmi Desemba 16, mwaka huu, baada ya kukatizwa kwa zaidi ya miezi sita. **RFI**



# Jeshi Uganda lazingira nyumba ya Bobi Wine

**Kampala,** UGANDA

KIONGOZI wa upinzani Uganda, Robert Kyagulanyi, maarufu Bobi Wine, ametuma picha ya polisi na jeshi wakionekana nje ya nyumba yake, kabla ya kampeni za uchaguzi mdogo unaotarajiwa kufanyika katika Wilaya ya Kayunga.

Rais Yoweri Museveni, anatarajiwa kutembelea katika Wilaya ya Kayunga, kumfanyia kampeni mgombea wa chama tawala anayewania nafasi ya uenyekiti.

**Vyombo vya habari Uganda, viliripoti kuwa polisi na jeshi pia walipelekwa Kayunga kabla ya kampeni za jana.**

Uchaguzi huo mdogo, umepangwa kufanyika kesho huku chama tawala na upinzani kwa pamoja, vinataka kuonyesha uwezo wao katika eneo hilo. Bobi Wine, ameshutumu Jeshi la Polisi kwa kujaribu kumzuwia kuondoka nyumbani kwake:

Vyombo vya habari Uganda, viliripoti kuwa polisi na jeshi pia walipelekwa Kayunga kabla ya kampeni za jana.

Awali Kayunga ilikuwa ni ngome ya chama tawala hadi mwenyekiti wa zamani aliyefanikiwa madarakani kuchaguliwa kutoka upinzani.

Chama tawala kinataka kurejesha tena kiti hicho na kimeahidi kuufanya mji huo kuwa manispaa, limeripoti gazeti la Daily Monitor. **BBC**



Mbunge wa Makindye Mashariki, Derrick Nyeko (watatu kushoto), akiwa na maofisa usalama eneo ambako vimewekwa vizuizi kwenye barabara, jirani na makazi ya kiongozi wa upinzani wa Chama cha National Unity Platform (NUP), Robert Kyagulanyi, mjini Magere, wilayani Wakiso, nchini Uganda, jana. **PICHA: MONITOR**

# Chakula cha msaada chaibwa Ethiopia

**Addis Ababa,** ETHIOPIA

KWA mara ya pili katika kipindi cha siku kadhaa, msaada wa chakula kwa ajili ya Waethiopia ambao wanakabiliwa na baa la njaa, umeibiwa kutoka katika ghala la Mpango wa Chakula Duniani (WFP), Kaskazini mwa Ethiopia, Umoja wa Mataifa (UN), umesema.

Msemaji wa UN, Farhan Haq, aliwaeleza wanahabari kwamba kundi la watu waliokuwa na silaha wanaoaminika kutoka jeshi la taifa la Ethiopia ama vikosi vyenye ushirika na jeshi, vilivamia eneo la kuhifadhi chakula la kamati ya kukabiliana na maafa ambalo lipo Kambolcha, na kuchukua malori 18 ya WFP kinguvu.

Alisema malori yaliyochukuliwa yalitumiwa na watu hao katika maeneo kadhaa kwa ajili ya shughuli zao binafsi, akisema malori 15 yamerejeshwa, matatu hayajapatikana.

Msemaji huyo aliongeza kusema kwamba ulinzi na usalama wa wafanyakazi wa UN na washirika wake bado unaendelea kuwa kipaumbele cha juu na wanataka wafanyakazi wao na washirika wake warejeshwe kwa haraka na wakiwa salama, pamoja na magari yaliyoibiwa.

WFP, imeifahamisha serikali kuu ya Ethiopia na mamlaka za kieneo katika mji wa Dessie, ambao msemaji alisema walisaidia katika kupatikana kwa malori matatu.

Miji hiyo ipo katika Mkoa wa Amhara, Kaskazini mwa Ethiopia, ambao umeshuhudia mahitaji ya msaada yakiongezeka katika miezi ya karibuni.

UN, unasema watu milioni 3.7 wa Amhara wanahitaji misaada ya kibinadamu kutokana na mgogoro baina ya vikosi vya serikali KJJ na vile vya eneo la Tigray (TPLF). **VOA**

# Kikosi wanasayansi kuchunguza Omicron A. Kusini

**Johannesburg,** AFRIKA KUSINI

KIKUNDI cha wanasayansi wa Urusi, kimewasili Afrika Kusini kufanya uchunguzi wa virusi vipya vya corona, Omicron.

Wizara ya Afya ya Urusi, imetuma ujumbe wa video kwenye Twitter wa wanasayansi hao wakiwasili, na kuongeza kuwa ndege waliyokuwamo imebeba maabara inayoweza kuhamishwa.

Kuwasili kwa wanasayansi hao wa Urusi, kunakuja siku mbili baada ya Rais wa Afrika Kusini, Cyril Ramaphosa kuwaalika wataalamu kutoka nchi mbalimbali kujiunga na wanasayansi nchini mwake, kuchunguza aina mpya ya omicron na hali zake tofauti za maumbile, huku naye akipata maambukizi mwanzoni mwa wiki hii. **BBC**

# GEITA GOLD, TRANSIT CAMP ZASONGA MBELE FA CUP

**Na Saada Akida**

TIMU ya Transit Camp na Geita Gold, zimefuzu mzunguko wa nne wa Kombe la Shirikisho la Azam (ASCF) maarufu FA Cup, baada ya kushinda michezo yao ya juzi iliyochezwa kwenye viwanja tofauti nchini.

**Transit Camp iliibuka na ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya Kawe Fresh mchezo uliochezwa uwanja wa Karume, Dar es Salaam.**

Akizungumza na gazeti hili jijini jana baada ya mchezo huo, Kocha Mkuu wa Transit Camp inayoshiriki Championship, Rajab Bwamkuu, alisema ushindi huo umetokana na vijana wake kujituma na kufuata maelekezo aliyowapa, hivyo anashukuru kwa kuweza kusonga mbele.

Alisema mbali na wachezaji wake kujituma, pia uzoefu wao umechangia kwa kiasi kikubwa kufanya vizuri na kupata ushindi katika mchezo huo dhidi ya Kawe Fresh.

"Kipindi cha kwanza hatukucheza vizuri hasa safu ya ulinzi, tukaruhusu bao hadi mapumziko walikuwa wakiongoza 1-0, lakini tulibadilika kipindi cha pili na kufanikiwa kusawazisha na kupata bao la pili," alisema Rajab.

Alisema wanaenda kujipanga vizuri kwa ajili ya mzunguko unaofuata kwa kuhakikisha wanaimarisha mbinu zao ili kupata matokeo mazuri na kuendelea kusonga mbele hadi kufikia malengo yao.

Naye Kocha Mkuu wa Kawe Fresh, Hussein Bunu alisema ameyakubali matokeo kwa kupoteza mchezo wao, hivyo wanakwenda kujipanga na mchezo ujao wa Ligi ya Kanda ya Dar es Salaam itakayoanza mapema mwezi huu.

"Sisi ni timu changa tuko ligi ya Mkoa, kupitia mashindano haya tumejifunza kitu na tumejijenga kwa kupata mechi kama hiyo, hivyo tunakwenda kujipanga zaidi," alisema Bunu.

Kwingineko, Geita Gold ilishinda mabao 4-0 dhidi ya DHB katika mchezo uliopigwa uwanja wa Nyankumbu, Geita.

Michezo mingine, Lindi United nayo ilikata tiketi ya kusonga mbele baada ya kuifunga Tanesco mabao 2-1 katika mchezo uliopigwa uwanja wa Ushirika mkoani Kilimanjaro.

Kimara iliondolewa katika michuano hiyo kwa mikwaju ya penalti 6-5 dhidi ya Top Boys, baada ya dakika 90 katika uwanja wa Jamhuri Dodoma kumalizika kwa suluhu.

Matokeo mengine; Catamine ilisonga mbele kwa mikwaju ya penalti 4-2 dhidi ya Blue Swallows baada ya dakika 90 za mchezo huo kumalizika kwa sare ya bao 1-1.




Kipa wa Biashara United, James Ssetuba, akiteta na mwamuzi Ahmed Aragija, baada ya kiungo wa Mtibwa Sugar, Baraka Majogoro (chini), kuchezewa madhambi kwenye mechi ya Ligi Kuu iliyopigwa Uwanja wa Manungu mkoani Morogoro Jumapili iliyopita. Mtibwa ilishinda 2-0. **NA MPIGAPICHA WETU**

# Simba Queens yataja mikakati yao Ligi Kuu

**Na Saada Akida**

WAKATI ikiwa imesalia wiki moja kuelekea kufunguliwa kwa pazia la Ligi Kuu ya Wanawake nchini kwa msimu wa 2021/22, inayotarajiwa kuanza Desemba 23, kikosi cha Simba Queens chini ya Kocha Mkuu, Sebastian Nkoma, kinaendelea na mazoezi makali kuhakikisha kinaanza vema kutetea ubingwa wao, imeelezwa.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, Kocha Sebastian alisema wamejiandaa vizuri kuhakikisha wanapata matokeo mazuri katika michezo yao mitano ya kwanza.

Alisema msimu huu utakuwa wa ushindani kwa sababu timu nyingi zimejiimarisha kwa kufanya usajili mzuri, lakini hata wao wamefanya maandalizi makubwa.

"Lengo kubwa la msimu huu ni kuhakikisha tunafanya vizuri katika michezo yote iliyopo mbele yetu kwa lengo la kuendelea kutetea ubingwa wetu ambao tumechukua kwa mara ya pili mfululizo," alisema kocha huyo.

# Arusha wang'ara Samia Taifa Cup

**Na Saada Akida**

WANARIADHA wa Mkoa wa Arusha wameng'ara katika mashindano ya Kombe la Taifa, ya Samia Taifa Cup yanayoedelea katika Uwanja wa Benjamini Mkapa, Dar es Salaam.

Katika nafasi ya kwanza kwa upande wa wanawake, Masalina Issa ameshika nafasi ya kwanza mbio za mita 5,000 huku Asha Salim akishika ya pili na mshindi wa tatu akiwa ni Sesilia Ginoka wote kutoka Arusha, ambao waliwashinda washiriki wengine ambao ni Anastazia Dolomangu wa Dodoma, Tunu Andrew (Singida), Jesca Raphael (Tabora), Ramla Fabian,(Dodoma) na Rebeka Machege wa Dar es Salaam .

Kwa upande wa wanaume mita 10,000, mshindi wa kwanza ni Kaposhi Laizaki kutoka Kilimanjaro na nafasi ya pili ikienda kwa Inyasi Sule wa Arusha.

Mbio za mita 800 kwa wanawake mshindi wa kwanza ni Aisha Lubuna kutoka Dodoma huku Mariam Salim wa Arusha akimaliza katika nafasi ya pili.

# Biashara United yaipania Nyota Academy kesho

**Na Shufaa Lyimo**

KLABU ya Biashara United, imesema licha ya kuvurugwa na matokeo mabaya waliyoyapata mwishoni mwa wiki baada ya kupoteza katika mechi ya Ligi Kuu Bara dhidi ya Mtibwa Sugar, wamejipanga vema kupata ushindi kwenye mchezo wa raundi ya tatu ya Kombe la Shirikisho la Azam (ASCF), maarufu FA Cup dhidi ya Nyota Academy ya Arusha.

Akizungumza na gazeti hili jana kwa njia ya simu kutoka Musoma mkoani Mara, Meneja Mkuu wa klabu hiyo, Frank Wabare, alisema ana uhakika wa kikosi chao kupata matokeo kesho kwenye mchezo.

"Baada ya kupata matokeo ambayo hatukuridhika nayo, kwenye mchezo wetu uliopita, kocha wetu ameahidi kurekebisha mapungufu yote aliyoyabaini ili kufanya vizuri kwenye mechi ijayo," alisema Wabare.

Meneja huyo alisema kocha wao anaendelea kufanyia kazi safu ya ushambuliaji ambayo inaonekana kuwa butu kutokana na kupoteza nafasi nyingi.

Wabare alisema wanaupa umuhimu mkubwa mchezo huo wa Kombe la Shirikisho wakiwa na lengo la kusonga mbele.

Alisema Ligi Kuu msimu huu ni ngumu na yenye ushindani kutokana na maandalizi yaliyofanywa na timu zote, kwa kuwa kila timu inahitaji matokeo kutokana na bonasi kubwa zilizotolewa na wadhamini haki za matangazo ya televisheni, Azam Media Limited.

Kwa upande wa hali ya wachezaji wao, alisema wanaendelea vizuri na kila mmoja morali ipo juu kuelekea mechi hiyo ya kesho.

Katika mechi iliyopita, Biashara United ilikubali kipigo cha mabao 2-0 dhidi ya Mtibwa Sugar kwenye mechi iliyopigwa uwanja wa Manungu mkoani Morogoro.

## ZISIKUPITE

### RUDIGER SAFI MADRID

REAL Madrid wanakaribia kumsajili mlinzi wa Chelsea, Antonio Rudiger, 28, baada ya mazungumzo mazuri na Mjerumani huyo kuhusu kujiunga nao bila malipo msimu ujao wa majira ya joto. ***(Guardian)***

### DELE KUONDOKA SPURS

KIUNGO Dele Alli, 25, huenda akafikia kikomo kwani kocha, Antonio Conte hamuoni mchezaji huyo katika mipango yake. ***(The Athletic, via Star)***

### ATAKIWA NEWCASTLE

NEWCASTLE wamemfanya mlinzi wa kati wa Lille, Sven Botman, 21, kuwa usajili wa kipaumbele katika dirisha la uhamisho la Januari, huku winga wa Manchester United, Jesse Lingard, 28, pia akiwa kwenye orodha ya Eddie Howe. ***(Guardian)***

### CAVANI KWENDA BRAZIL

KAKA wa Edinson Cavani ameashiria kuwa mshambuliaji huyo anakaribia kuondoka Manchester United, huku kukiwa na uwezekano wa kuhamia Brazil. ***(Manchester Evening News)***

### BARCA, JUVE KWA CAVANI

BARCELONA, Juventus na klabu ya Corinthians ya Brazil wana nia ya kumsajili Edinson Cavani wa Manchester United. ***(Marca)***

### DIAZ AGOMBEWA ENGLAND

MANCHESTER United wako tayari kushindana na wapinzani wa Ligi Kuu England, Liverpool na Manchester City katika kumsaka winga wa Porto, Luis Diaz, 24. ***(Fichajes, via Team Talk)***

### BURNLEY YAJIPANGA JANUARI

KOCHA wa Burnley, Sean Dyche amesema klabu hiyo haitatumia kiasi kikubwa katika dirisha la uhamisho la Januari. ***(Talksport)***

### DAVIS LULU NOTTINGHAM

MSHAMBULIAJI aliyesahaulika wa Aston Villa, Keinan Davis, 23, ameibuka kama shabaha ya uhamisho wa Januari na klabu inayoshiriki Ligi Daraja la Kwanza ya Nottingham Forest. ***(Birmingham Live)***


### MOURA AWANIWA BRENTFORD

KLABU ya Brentford imewasiliana na Braga kuhusu uwezekano wa kumnunua beki wa kushoto wa Ureno, Francisco Moura, 22, Januari. ***(Sun)***

### LAPORTA ATETA NA RAIOLA

RASI wa Barcelona, Joan Laporta alifanya mkutano na wakala, Mino Raiola nchini Italia kwa ajili ya kiungo, Paul Pogba, 28, ambaye mkataba wake kule Manchester United unamalizika kipindi cha majira ya joto kijacho. ***(Fabrizio Romano, via Mail)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# RANGNICK: MARTIAL NIAMBIE KAMA UNATAKA KUONDOKA

● ● ● Siwasiliani na wakala kupitia vyombo vya habari, mchezaji hajazungumza na mimi au kuhusu hilo, hivyo...

**MANCHESTER,** England

RALF Rangnick amemwambia Anthony Martial kumjulisha yeye binafsi kama anataka kuondoka Manchester United, kuliko kupitia kwa wakala wake.

Wakala wa mchezaji huyo wa kimataifa wa Ufaransa, Philippe Lamboley, alisema Ijumaa kwamba mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26, anaangalia uwezekano wa kujiunga na klabu mpya Januari kutokana na kukosa muda wa kutosha kucheza.

**Martial amecheza dakika 358 kwa 'Mashetani Wekundu' hao katika mashindano yote msimu huu – katika mechi 20 akianza mara nne tu.**

"Anthony anataka kuondoka klabuni Januari," alisema Lamboley akiiambia Sky Sports.

"Anataka kucheza. Hataki kubaki hapa Januari na atazungumza na klabu hivi karibuni."

Lakini habari za mchezaji huyo wa zamani wa Monaco kutaka kuondoka United zimekuja kama mshangao kwa kocha mpya wa muda, Rangnick.

"Siwasiliani na wakala kupitia vyombo vya habari," alisema Rangnick.

"Mchezaji hajazungumza na mimi au kuhusu hilo.

"Nikiwa mkweli, kile ambacho wakala wake anazungumza kupitia vyombo vya habari hakinivutii mimi. Anatakiwa kwa mchezaji mwenyewe."

CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 783

MECHI KALI
HOME AWAY
ARSENAL
2.24 | 3.41 | 3.12
WEST HAM

KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#,
CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa vodacom m-pesa
halopesa airtel money ZANTEL EZYPESA
SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249 HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# PEDRI: BARCA ITARUDI KWENYE UBORA WAKE



**BARCELONA,** Hispania

PEDRI anaishi katika ndoto ya Barcelona na ana matumaini kuiongoza klabu hiyo kwenye mafanikio makubwa baada ya kupokea tuzo yake ya Golden Boy, Jumatatu.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 19, alichaguliwa kuwa mchezaji bora kijana barani Ulaya, akimshinda Jude Bellingham.

Alifurahia kuingia kikosi cha kwanza pale Camp Nou baada ya kuanza kuichezea Septemba mwaka jana na akaenda kucheza mechi (52) nyingi zaidi kuliko mchezaji yeyote wa Barca.

Pedri alikuwa mchezaji wa kwanza kuichezea Hispania kwenye mashindano makubwa katika Euro 2020.

Nyota huyo kijana ambaye kwa sasa yupo nje akisumbuliwa na majeraha ya paja, amekubali kwamba, mambo yamekuwa magumu kwa timu yake, lakini anaamini hali itabadilika.

"Kuwa hapa Barcelona ni ndoto kwa upande wangu," alisema akinukuliwa na AS. "Hii ni klabu bora duniani, ingawa lazima tuanze kuonyesha ubora wetu uwanjani na kuiongoza Barca kwenye ubora inayostahili."

# *Dele sasa kuondoka Tottenham Januari*

**MILAN,** Italia

DELE Alli yuko huru kuondoka Tottenham Hotspur Januari baada ya kupoteza nafasi yake chini ya Jose Mourinho na hakuweza kuondoka kwa mkopo licha ya kuhusishwa na Paris Saint-Germain.

Muda wa Nuno Espirito Santo pale Spurs ulionekana kana kwamba ungemruhusu Dele kurejea katika kiwango chake, lakini amerudi nyuma chini ya kocha wa sasa Antonio Conte.

Hapo awali, Spurs walisita kumruhusu kiungo huyo aondoke na Daniel Levy alipambana na Paris Saint-Germain mwaka 2020 na Januari 2021, lakini sasa Fabio Paratici, Mkurugenzi Mkuu na Conte wote wamekubaliana kwamba milango iko wazi kuondoka.

Kwa mujibu wa The Athletic klabu zinasita kufika dau la Spurs kwa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25, na mkataba wake ukiendelea hadi 2024.

Chini ya Conte, Dele amecheza mechi moja pekee ya Ligi Kuu England, ambayo ilikuja kama mbadala katika ushindi wao dhidi ya Leeds United.



# LWANDAMINA AFUNGUKA KUFUKUZWA



**Na Dennis Fussi**

KOCHA George Lwandamina amesema si jambo la kushangaza kwa kocha kufukuzwa kazi, kwani ni kawaida kwa ulimwengu wa soka na yeye hana tatizo kutupiwa virago vyake na Azam FC.

Lwandamina aliondolewa pamoja na msaidizi wake, Vivier Bahati juzi, baada ya kikosi hicho kuanza vibaya kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu wa 2021/22. Lwandamina amesema: "Nimepokea taarifa hiyo, na kwangu si jambo la kushangaza, kwani hutokea duniani kote, haya ni maisha yetu ya mpira."

Kocha huyo mwezi uliopita alisaini mkataba mpya wa mwaka mmoja, lakini mabosi wake wameamua kuuvunja mkataba huo, kwa kutazama maslahi ya kikosi chao.

Azam hadi sasa ipo nafasi ya saba kwenye msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara ikiwa na pointi 11, ikishinda michezo mitatu, sare mbili na kupoteza mechi tatu.

# Makocha kibao watajwa kuinoa Mtibwa Sugar

**Na Dennis Fussi**

UONGOZI wa Mtibwa Sugar unatarajia kumtangaza kocha mpya wa kuchukua mikoba ya Joseph Omog ndani ya siku chache zijazo, kwa mujibu wa Ofisa Habari wa timu hiyo, Thobias Kifaru.

Awali, taarifa zilibainisha kwamba, Salum Mayanga (pichani), ndiye amepewa mikoba hiyo baada ya kuvunja mkataba wake na Tanzania Prisons ya Mbeya, lakini Kifaru ameliambia gazeti hili kuwa, bado wanaendelea kuchambua majina ya makocha wa hapa nchini na nje ya nchi.

"Kuhusu Mayanga siwezi kuthibitisha hilo, kwani yeye ni muajiriwa wa kiwanda cha Mtibwa na huwa anaruhusiwa tu kwenda kuzinoa timu na mkataba wake ukimalizika huwa anarudi nyumbani," alisema Kifaru.

Aliongeza: "Kwa sasa tunaendelea kuchambua majina ya makocha wa hapa ndani na wengine kutoka nje ya nchi na ndani na siku chache zijazo tutamtangaza rasmi kocha mkuu wa Mtibwa."

Aidha, alisema Omog ambaye ni raia wa Cameroon wamemalizana naye na leo ataondoka rasmi nchini kurudi kwao na tayari wameshamkatia tiketi.

Kwa mujibu wa kifaru, Mtibwa sasa inaongozwa kwa muda na Awadh Juma akisaidiana na Shaban Nditi ambaye alikuwa nahodha wa zamani wa timu hiyo.

Mtibwa hadi sasa imepata ushindi mmoja tu katika mechi nane ilizocheza kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara na inashika nafasi ya 15 ikiwa na pointi tano.




3,781,040

JACKPOT MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 18/12/2021 | 18:00 | Bristol City vs Huddersfield | 2.69 | 3.18 | 2.54 |
| 02. 18/12/2021 | 18:00 | Watford vs Crystal Palace | 2.89 | 3.34 | 2.41 |
| 03. 18/12/2021 | 20:30 | Leeds vs Arsenal | 2.97 | 3.41 | 2.32 |
| 04. 18/12/2021 | 22:45 | Cagliari vs Udinese | 3.00 | 3.29 | 2.37 |
| 05. 18/12/2021 | 23:00 | Sevilla FC vs Atletico Madrid | 2.65 | 3.00 | 2.85 |
| 06. 19/12/2021 | 15:00 | Everton vs Leicester | 2.75 | 3.30 | 2.55 |
| 07. 19/12/2021 | 16:00 | Granada vs Mallorca | 2.49 | 3.14 | 2.94 |
| 08. 19/12/2021 | 16:00 | Fuenlabrada vs Real Oviedo | 2.90 | 3.05 | 2.45 |
| 09. 19/12/2021 | 17:00 | Spezia vs Empoli | 2.40 | 3.49 | 2.79 |
| 10. 19/12/2021 | 17:30 | SC Freiburg vs Bayer Leverkusen | 2.79 | 3.44 | 2.40 |
| 11. 19/12/2021 | 18:00 | Zaragoza vs Tenerife | 2.38 | 3.08 | 2.98 |
| 12. 19/12/2021 | 20:30 | Getafe vs Osasuna | 2.49 | 2.90 | 3.20 |
| 13. 19/12/2021 | 22:45 | AC Milan vs Napoli | 2.37 | 3.41 | 2.91 |

MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMATANO - 15 - DESEMBA 2021

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 17:00 | 3821 | Verona vs Empoli | 1.86 | 3.65 | 3.79 |
| 18:15 | 1830 | Lamia vs Volos | 2.41 | 3.30 | 2.80 |
| 18:15 | 2958 | PAS Giannina vs PAOK | 3.80 | 3.45 | 1.91 |
| 19:00 | 4098 | Cukaricki St vs FK Radnicki 1923 | 1.17 | 6.37 | 11.58 |
| 19:00 | 4224 | Slavia Prague vs Zlin | 1.11 | 7.52 | 15.42 |
| 20:00 | 1039 | Rakow Czestochowa vs Gornik Zabrze | 1.80 | 3.46 | 3.94 |
| 20:00 | 1298 | AZ Alkmaar vs Heracles Almelo | 1.43 | 4.33 | 5.97 |
| 20:00 | 2451 | Harkemase Boys vs Waalwick | 6.16 | 4.62 | 1.39 |
| 20:00 | 3890 | Vitesse Arnhem vs Sparta Rotterdam | 1.62 | 3.80 | 4.52 |
| 20:00 | 4358 | Twente vs Feyenoord | 3.67 | 3.62 | 1.81 |
| 20:00 | 4412 | Cagliari vs Cittadella | 1.79 | 3.65 | 4.14 |
| 20:00 | 4544 | Istra vs Dinamo Zagreb | 8.48 | 4.82 | 1.29 |
| 20:30 | 1428 | Monchengladbach vs Eintracht Frankfurt | 1.97 | 3.69 | 3.49 |
| 20:30 | 1784 | Apollon Smyrnis vs Panathinaikos | 4.73 | 3.75 | 1.68 |
| 20:30 | 3421 | Atromitos vs Olympiakos | 7.31 | 4.54 | 1.39 |
| 20:45 | 2182 | Mechelen vs KAA Gent | 3.70 | 3.65 | 1.88 |
| 20:45 | 4017 | Zulte Waregem vs Union Saint Gilloise | 5.92 | 4.73 | 1.44 |
| 21:00 | 1142 | Bergantinos CF vs Rayo Vallecano | 21.64 | 8.26 | 1.10 |
| 21:00 | 5254 | Brann vs Jerv | 1.71 | 3.95 | 4.50 |
| 21:00 | 5990 | CE Andratx vs Sevilla FC | 34.62 | 9.89 | 1.06 |
| 21:30 | 3631 | Steaua Bucuresti vs Rapid Bucuresti | 1.63 | 3.72 | 5.09 |
| 21:30 | 4687 | Leonesa vs Leganes | 3.25 | 3.16 | 2.22 |
| 22:00 | 1263 | SBV Excelsior vs Groningen | 2.94 | 3.37 | 2.16 |
| 22:00 | 1283 | Sporting Gijon vs Alcorcon | 1.61 | 3.64 | 5.51 |
| 22:00 | 1341 | Ponferradina vs UD Ibiza Eivissa | 2.07 | 3.15 | 3.64 |
| 22:00 | 3882 | Benfica vs Covilha | 1.08 | 9.54 | 23.85 |
| 22:00 | 4051 | CD Castellon vs FC Cartagena | 3.31 | 3.16 | 2.19 |
| 22:00 | 5188 | Valladolid vs Las Palmas UD | 2.07 | 3.21 | 3.56 |
| 22:30 | 1541 | Union Berlin vs SC Freiburg | 2.41 | 3.29 | 2.89 |
| 22:30 | 1754 | Crystal Palace vs Southampton | 2.13 | 3.36 | 3.41 |
| 22:30 | 3097 | BSC Young Boys vs FC Basel | 1.61 | 4.25 | 4.55 |
| 22:30 | 3303 | Augsburg vs RB Leipzig | 6.00 | 4.60 | 1.47 |
| 22:30 | 3567 | Burnley vs Watford | 2.12 | 3.40 | 3.40 |
| 22:30 | 4237 | Legia Warszawa vs Zaglebie Lubin | 1.70 | 3.71 | 4.15 |
| 22:30 | 4605 | Brighton vs Wolverhampton | 2.33 | 3.05 | 3.30 |
| 22:30 | 4630 | Borussia Dortmund vs Greuther Furth | 1.10 | 9.35 | 18.91 |
| 22:30 | 5970 | Bayer Leverkusen vs Hoffenheim | 1.81 | 4.07 | 3.77 |
| 22:45 | 3512 | Ross County vs Celtic | 8.30 | 5.33 | 1.30 |
| 22:45 | 3946 | Rangers vs St Johnstone | 1.14 | 7.10 | 16.76 |
| 22:45 | 5128 | Barrow vs Ipswich | 3.70 | 3.36 | 1.97 |
| 23:00 | 1080 | Atletico Sanluqueno vs Villarreal | 9.30 | 4.95 | 1.31 |
| 23:00 | 1213 | Unionistas CF vs Elche | 7.71 | 4.84 | 1.35 |
| 23:00 | 1269 | Arsenal vs West Ham | 2.24 | 3.41 | 3.12 |
| 23:00 | 1540 | PSV Eindhoven vs Fortuna Sittard | 1.13 | 7.14 | 13.51 |
| 23:00 | 2924 | Standard Liege vs Kfco Wilrijk | 1.73 | 3.85 | 4.24 |
| 23:00 | 3196 | Fiorentina vs Benevento | 1.29 | 5.31 | 9.05 |
| 23:00 | 3558 | Ajax vs BVV Barendrecht | 1.01 | 20.29 | 38.64 |
| 23:00 | 3947 | Tenerife vs Eibar | 2.45 | 3.05 | 2.95 |
| 23:00 | 5220 | GO Ahead Eagles vs Roda Kerkrade | 1.81 | 3.56 | 3.75 |
| 23:00 | 5270 | OH Leuven vs Brugge | 5.30 | 4.22 | 1.54 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# Michezo

Jumatano Desemba 15, 2021

Nipashe




Rangnick: Martial niambie kama unataka kuondoka UKURASA 21

# Yanga SC na hasira kwa Ihefu, Katwila aionya

●●● Asema haitakuwa rahisi, kukumbushia zilipotoana kwa matuta Kombe la FA 2018, Nabi naye...

**Saada Akida na Adam Fungamwango**

WANAFAINALI wa Kombe la Shirikisho la Azam (ASFC), maarufu FA Cup msimu uliopita, Yanga, leo watakuwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa kuanza safari yao mpya msimu huu watapoikaribisha Ihefu FC kwenye mchezo wa raundi ya tatu ya michuano hiyo.

**Mechi hiyo itakayopigwa saa moja usiku, itachezwa siku nne tu baada ya Yanga kutoka suluhu dhidi ya watani zao wa jadi, Simba kwenye uwanja huo huo katika mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara.**

Kocha Mkuu wa Yanga, Nasreddine Nabi (pichani) amesema kikosi chake kipo imara na wanaenda kupambana kutafuta matokeo mazuri katika mchezo huo ambao ni muhimu kwao kushinda.



Akizungumza na Nipashe, Nabi alisema katika mashindano hakuna timu ndogo kila mechi kwao ni muhimu kupata matokeo mazuri hasa ukizingatia michuano hii ni ya mtoano na mshindi hupata nafasi ya kuwakilisha nchini, Kombe la Shirikisho Afrika.

"Hakuna mechi rahisi, kila mmoja anahitajj matokeo mazuri tumefanyia kazi mapungufu yaliyojitokeza katika mechi iliyopita ikiwamo kutengeneza nafasi na kuzitumia vema ili kupata ushindi," alisema Nabi.

Kwa upande wa Kocha wa Ihefu FC, Zuberi Katwila, alisema wamefanya maandalizi mazuri na wanaiheshimu Yanga ni timu kubwa na ina wachezaji wazuri, lakini hawataogopa majina ya nyota hao na wataingia uwanjani kupambana mwanzo mwisho.

"Mechi itakuwa na ushindani mkubwa kwa sababu kila mmoja anahitaji matokeo ili kusonga mbele, ukizingatia wapinzani wetu wameimarika vizuri, lakini tumejiandaa vizuri kwenda kuleta ushindani," alisema Katwila.

Mechi hiyo ya leo ya raundi ya tatu ya Kombe la FA, itakumbushia mchezo wa mwaka 2018, ambao Yanga ilipata upinzani mkali kutoka kwa timu hiyo yenye maskani yake Mbarali, Mbeya, wakati huo kabla haijapanda Ligi Kuu Tanzania Bara msimu wa 2020/21, kabla ya kushuka tena msimu huo huo.

Mechi hiyo kali iliyopigwa Januari 30, 2018 kwenye uwanja wa Sokoine, Yanga ilipata wakati mgumu ikionekana imeshalala, ikisawazisha bao dakika za majeruhi na kushinda kwa mikwaju ya penalti 4-3.

Baadaye Ihefu ilipanda msimu 2020/21, lakini ikateremka msimu huo huo uliomalizika na sasa ipo ngazi ya Championship.

Pamoja na mechi hiyo, Azam FC nayo itakuwa kwenye uwanja wa Azam Complex, Chamazi kucheza dhidi ya maafande wa Green Warrios kwenye mechi ya raundi ya tatu ya Kombe la FA, itakayochezwa saa 10:00 jioni kwa saa za Afrika Mashariki.

Azam itacheza mechi hiyo bila George Lwandamina, aliyejiuzulu nafasi yake juzi kwa kile kilichoelezwa kuwa ni kwa maslahi ya klabu.

Kikosi cha Azam FC kitakuwa chini ya Abdihamid Moalim kwa mara ya kwanza, akikaimu nafasi ya Kocha Mkuu.

Moalim hivi karibuni alitangazwa Mkurugenzi wa Ufundi wa klabu hiyo.

NA WAJE TU...



Wachezaji wa Yanga wakiwa mazoezini. Leo timu hiyo itaikaribisha Ihefu FC kwenye mechi ya raundi ya tatu ya Kombe la FA itakayopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa majira ya saa moja usiku. **PICHA: MAKTABA**

## Simba, TFF, Bodi ya Ligi kuyamaliza

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Simba imesema kuwa itakaa na Shirikisho la Soka nchini (TFF), pamoja na Bodi ya Ligi ili kumaliza tofauti zilizojitokeza hivi karibu, ikiwamo kuzuiwa kuingia uwanjani kwa Ofisa Mtendaji Mkuu, Barbara Gonzalez kwenye mechi dhidi ya Yanga Jumamosi iliyopita.

Mwenyekiti wa Bodi ya Klabu hiyo, Salim Abdallah 'Try Again', amesema wameiandikia barua TFF na Bodi ya Ligi kuwasilisha malalamiko yao na kwa bahati nzuri wamekubali kukaa kuzungumza ili kuondoa kero na tatizo hilo ili lisijirudie tena.

"Sasa tunakwenda kutafuta suluhu, wamekubali kukaa na kuzungumza, hivyo nawasihi wanachama na mashabiki wa Simba watulie, litafikia muafaka na baada ya vikao vyetu tutatoa ufafanuzi ulionyooka, kwa sasa Wanasimba wajue kuwa viongozi wao wanalishughulikia suala hilo," alisema.

Alisema hiyo haikuwa mara ya kwanza kwa Barbara kuzuiwa, kwani hata yeye, na Mshauri wa Mwekezaji wa Klabu ya Simba, Crescentius Magori walikumbana na kadhia hiyo.

Kuhusu ujenzi wa uwanja, Mwenyekiti huyo alisema watakaa kikao na hivi karibuni watatoa utaratibu wa wanachama kuchangia.

Kuzuiwa kwa Barbara ndiko kulikoibua hisia za mashabiki wa Simba kutaka kuchangia ili kuondokana na kadhia hiyo.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >